SportPesa
TZS. 1,089,062,840
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**WATOTO** wabakwa, walawitiwa siku 90


Nipashe TESA
Jumanne Machi 29, 2022 TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
KUTOKA MRADI ELIMU JUMUISHI SHY...
Magumu ya walimu wasio na stadi madarasani kwa wenye ulemavu
Wanafunzi mkondo wa PCM waonyesha maajabu kuwapiku wahandisi kompyuta
ELIMU
NA DK. CAESAR JJINGO, KAMPALA
Ufundishaji Kiswahili Uganda unavyoleta mkanganyiko ndani
Kitendawili cha saa chawatoa jasho
TENDERS
GOVT REGISTERS, CLEARS 2,000 NGOS, LIST ON P4
New Vision
KISWAHILI COMPULSORY FOR O'LEVEL

UKURASA 11

# Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumanne Machi 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580899
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Ajali ilivyokatiza uhai wa Prof. Ngowi

**ALITATHMINI** uhusiano wa ajali na uchumi. Wengine 13 wafa...*Eendelea Uk. 2 & 3*


Sehemu ya mabaki ya gari la Profesa Honest Ngowi baada ya kuangukiwa na kontena mkoani Pwani na kusababisha kifo chake. **PICHA: MTANDAO**


Profesa Honest Ngowi

## KIKOSI KAZI CHATEGWA KUHUSU KATIBA MPYA

UKURASA 3



## Othman: Sheria ya uchochezi ni kandamizi

UKURASA 4



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, akizindua huduma mpya ya NMB Pesa Wakala jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Kaimu Ofisa Mkuu Udhibiti na Utekelezaji wa NMB, Oscar Nyirenda, Mkuu wa Idara ya Bidhaa, Aloyce Maro (kulia) na Ofisa Mkuu Teknolojia na Mabadiliko ya Digitali, Kwame Makundi (wapili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** CAF YAISHUSHIA RUNGU BERKANE MECHI SIMBA UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6



# Ajali ilivyokatiza uhai wa Profesa Ngowi

**Na Waandishi Wetu**

WATU 14 wamefariki dunia katika ajali tatu tofauti zilizotokea mkoani Pwani, Mbeya na Simiyu huku wengine 14 wakijeruhiwa.

Waliofariki ni pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe kampasi ya Dar es Salaam, Profesa Honest Ngowi (55), katika ajali iliyohusisha magari matatu kugongana na kuua wawili akiwamo dereva wa Prof. Ngowi, Innocent Grerson (33).

Akizungumza na waandishi wa habari jana Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo alisema ajali hiyo ilitokea majira ya saa 12 asubuhi eneo la Miwaleni Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.

Akizungumzia ajali hiyo, Kamanda Lutumo alisema gari namba T.608 AGV likiwa na tela lenye namba T.317 AQM aina ya Scania likiendeshwa na Raymond Kimaro (36) mkazi wa Ubungo kutoka nchini Kongo kwenda Dar es Salam, lilihama upande wake wa barabara na kugonga gari T.256 CMF aina ya Noah iliyokuwa ikitokea Dar es Salam kwenda Morogoro.

Alisema baada ya Scania hiyo kugonga Noah ilisababisha kontena kuchomoka na kuangukia gari SU 38223 aina ya Toyota Land Cruiser, iliyokuwa ikitokea Dar es Salaam kwenda Morogoro iliyokuwa ikiendeshwa na Innocent Gerson na kusababisha vifo vya watu wawili.

Aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni Raymond Kimaro, dereva wa lori na Abdallah Mohamed (33), mkazi wa Dar es Salam ambaye ni dereva wa Noah.

"Chanzo cha ajali kinachunguzwa, hata hivyo uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa ni uzembe wa dereva wa gari aina ya Scania kuhama upande wake wa barabara na kugonga Noah na kusababisha kontena kuchomoka na kuliangukia Toyota Land Cruiser," alisema Kamanda Lutumo.

Alisema mwili wa marehemu Prof. Ngowi umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani Tumbi na mwili wa dereva Innocent ukiwa umehifadhiwa katika kituo cha afya Mlandizi.

Majeruhi wa ajali hiyo wametibiwa na hali zao ni nzuri huku mtuhumiwa Raymond akishikiliwa na polisi kwa hatua zaidi.

Kuhusu makontena alisema wapo wataalamu wanayakagua kabla ya kutoka bandarini kuhakikisha kama yamefungwa vizuri kabla ya kuanza safari, na kwamba lililoangukia gari hilo tatizo halikuwa katika ufungaji lilichomoka baada ya ajali.

Mfanyakazi wa Mochwari ya Hospitali ya Tumbi, Monica Martine, alisema walipokea mwili wa Prof. Ngowi majira ya saa 1:30 asubuhi.

Monica alisema Prof. Ngowi alipelekwa katika hospitali hiyo kama majeruhi, lakini baada ya uchunguzi ilibainika ameshafariki na mwili wake ulikuwa na majeraha katika maeneo mbalimbali ya mwili wake makubwa yakiwa katika maeneo ya kichwani.

Mdogo wa marehemu, Juvenalis Ngowi alisema baada ya kupata taarifa ya ajali walifika katika hospitali hiyo na kugundua kuwa ndugu yao amefariki, kwa sasa wanaendelea kuwasiliana na familia na mwajiri kwa ajili ya taratibu za mazishi.

**AJALI YA TREKTA, SCANIA, BAJAJI**

Watu saba wamefariki dunia na wengine wanane kujeruhiwa baada ya kupata ajali iliyohusisha trekta, lori aina ya Scania pamoja na bajaji, juzi saa 1:00 usiku katika Barabara Kuu ya Bariadi-Maswa eneo la Kidulya, Wilaya ya Bariadi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Bariadi, Marco Igenge alisema, kati ya waliopoteza maisha sita walikufa papo hapo na mmoja alifariki wakati akipatiwa matibabu.

Ajali hiyo ilihusisha Scania yenye namba za usajili T172 AUP ikitokea Maswa kwenda Bariadi iliyogongana na bajaji MC 426 CFQ na kusababisha vifo pamoja na majeruhi hao.

Kaimu Mganga Mfawidhi aliwataja watu waliopoteza maisha kuwa ni Joseph Nsungi (31), Lameck Sayi (32), Pagi Hima (16) na Joseph Nzumbi (22).

Wengine ni Shinda Maige (17), Susa Sayi (18), Masunga Dotto (32), dereva wa bajaji.

Aliwataja majeruhi kuwa ni Robert Samwel (27), Habi Boniface (18), Mayunga Salum (22) na Manjale Joseph (22), Sitta Samwel (21).

Alisema kuwa miili ya marehemu imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti na majeruhi wanaendelea kutibiwa na baadhi wameanza kuruhusiwa.

"Baada ya tukio kutokea, tuliamua kuwaita madaktari na wahudumu wengine ambao hawakuwa zamu usiku ili kuweza kunusuru majeruhi maana hali ilikuwa mbaya, kazi kubwa ilifanyika na kufanikiwa kuwahudumia wote majeruhi na hali zao kwa sasa ni nzuri," alisema Igenge.

Robert Samwel, mmoja wa majeruhi akizungumza na waandishi wa habari, alisema chanzo cha ajali ni trekta ambalo halikuwa na taa wala viakisi mwanga na kusababisha dereva wa lori kutoliona.

Alisema dereva akiwa kwenye mwendo kasi, ghafla alishtuka amelifikia trekta na katika harakati za kulikwepa aliivamia bajaji ambayo ilikuwa kwenye eneo lake sahihi.

"Ile bajaji ilifunikwa na lori, sisi tulikuwa kwenye hilo lori na tulikuwa na mzigo wa tofali tukizitoa Maswa kuja Bariadi, baada ya ajali wote tulijikuta chini tukiwa tumefunikwa na tofali," alisema Samwel.

Samola Nola Shuhuda wa ajali hiyo, alisema kuwa wananchi waliokuwapo wakati ajali inatokea walifanya kazi kubwa ya kuokoa baadhi ya watu huku wakifankiwa kuzima moto ambao uliwaka baada ya bajaji kugongwa

**WATANO WAFARIKI LORI KUFELI BREKI**

Watu watano wamefariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa baada ya lori la mizigo lililokuwa limesheheni vifaa vya ujenzi kufeli breki kwenye mteremko wa Mlima Iwambi na kuparamia magari madogo matatu, bajaji moja, pikipiki na watembea kwa mguu katika mji wa Mbalizi, mkoani hapo.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia jana baada ya lori hilo kusababisha madhara hayo lilipoteza mwelekeo na kupinduka na kumwaga vifaa yakiwamo mabati na mipira ya maji.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya Ifisi, Dk. Hamis Ally, alisema katika hospitali hiyo walipokea maiti watano na majeruhi wanne ambao walikuwa na hali tofauti.

Aliwataja waliofariki kwenye ajali hiyo kuwa ni Mashak John (41), Mussa Msyani (26), Noah Japhet (26) na Shusa Mzumbwe (41), wote wakazi wa Mbalizi pamoja na Jeremiah Kenedy (38) mkazi wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe.

Vilevile, aliwataka majeruhi wa ajali hiyo kuwa ni Emmanuel Makunganya (47) na Sarah Makunganya (45) ambao ni mume na mke na wakazi wa Mbalizi ambao walitibiwa na kuruhusiwa.

"Lakini majeruhi wengine ni Shukurani Gunza (35), mkazi wa Mwanjelwa jijini Mbeya na Aledi Aledi (28), mkazi wa Mbalizi ambao mpaka sasa bado wanaendelea na matibabu hapa hospitali na hali zao zinaendelea kuimarika," alisema Dk. Ally.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo walisema lori hilo lilikuwa halijawasha taa wala halikuwa linapiga honi sababu iliyofanya watu waliopata madhara hasa watembea kwa miguu na madereva bodaboda kutoliona.

Mmoja wa mashuhuda hao, Paul Msangawale, alisema alikuwa jirani na eneo lilipoangukia lori hilo akiwa anaozungumza na mmoja wa madereva bodaboda ili ampeleke sehemu alikokuwa anataka kwenda kulala.

Alisema kabla hawajamaliza mazungumzo ndipo wakasikia kishindo na walipogeuka walikuta tayari lori hilo limeshaanguka na kutimua vumbi ambalo liliwatisha wakiamini kuwa ilikuwa ni gesi.

"Tulipoona gesi (vumbi) inatimka tuliamua kukimbia na kukaa mbali maana tulihisi ni hatari, lakini baada ya kutulia tuliamua kwenda na ndipo tukaanza kuwasaidia waliokuwa wameumia," alisema Msangawale.

Mmoja wa majeruhi waliolazwa katika hospitali hiyo, Shukurani Gunza, alisema baada ya ajali hiyo yeye alikuwa miongoni mwa walioenda kuokoa majeruhi na alimbeba mmoja wa majeruhi kumpeleka hospitali.

Alisema wakati wanaelekea hospitali walipata ajali ya kugongwa na gari na yeye akajeruhiwa, lakini aliyekuwa majeruhi alifariki palepale na wasamaria wema walimsaidia kumsindikiza hospitali.

Alisema mpaka sasa hajui gari iliyowagonga kwa kuwa alikuwa amepoteza fahamu, lakini anaendelea vizuri baada ya kupata matibabu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alikiri kutokea kwa ajali hiyo na chanzo ni mwendokasi wa lori.

***Imeandikwa na Julieth Mkikeri (KIBAHA), Happy Severine (SIMIYU) na Nebart Msokwa (MBEYA)***

# Watoto wabakwa, walawitiwa siku 90

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATOTO 10 wakazi wa Kata ya Mhongolo, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamebakwa na kulawitiwa kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita na wengine wawili wakiliwa na fisi.

Waliofanyiwa vitendo hivyo vya ukatili wanakadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka sita hadi 12 wa jinsia ya kike na walikutwa na mkasa huo baada ya kuagizwa na wazazi wao dukani nyakati za usiku.

Watoto wawili wa kike walioliwa na fisi wanatoka katika kata za Ngogwa na Wendele huku sababu ikitajwa kuwa ni kutokana na kuwapo mashamba makubwa ambayo wanyama hao wanajificha.

Mkaguzi wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto, Tiho Masatu, aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu.

Alisema wazazi na walezi wamekuwa wakichangia kusababisha watoto wao wa kike kufanyiwa vitendo vya kikatili hususani kubakwa na kulawitiwa na watu wasiojulikana kwa kuwaagiza nyakati za usiku kwenda dukani kufuata mahitaji ya nyumbani.

"Vitendo vya ubakaji na ulawiti vimekithiri sana katika kata ya Mhongolo eneo la mtaa wa Mbulu na sababu kubwa inaonyesha ni vitendo vya wazazi kuwa na tabia ya kuwatuma watoto madukani hususani nyakati za usiku," alisema Masatu.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wanakuwa makini katika kulinda watoto wao hususani wa jinsia ya kike ili kuepukana na vitendo hivyo kwa kuwa vimekuwa vikiwaathiri na kushindwa kuendelea na masomo yao shuleni.

Kuhusu watoto kuliwa na fisi, Masatu alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na idara ya wanyamapori wameanzisha msako wa kuwatafuta wanyama hao ili kuwatokomeza.

Hata hivyo, alisema mpaka sasa hakuna hata mnyama mmoja aliyekamatwa na kuuliwa na kwamba wamekuwa wakifanya kazi hiyo mara kwa mara.

Masatu aliitaka jamii kuacha kuhusisha matukio hayo na imani za kishirikiana na kuwataka kutoa ushirikiano ili kuhakikisha wanawatokomeza wanyama hao.

# Wadau wamlilia Profesa Ngowi

**Na Waandishi Wetu**

WADAU mbalimbali ikiwamo wachumi, wanahabari na wanasiasa wamemwelezea kwa namna tofauti Profesa Honest Ngowi (55), aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe kampasi ya Dar es Salaam, wakisema kifo chake ni pigo kwa taifa kutokana na umahiri wake wa uchambuzi, uwasilishaji utafiti na mwelimishaji wa masuala ya kiuchumi.

Walizungumza hayo na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, baada ya taarifa za kifo cha Prof. Ngowi kuthibitishwa kutokea Miwaleni, wilayani Kibaha, mkoani Pwani, baada ya kontena kuangukia gari waliyokuwa wakisafiria wakati wakielekea mkoani Morogoro kwenye kikao.

Katika makundi mbalimbali ya wanahabari mtandaoni wamemwelezea Prof. Ngowi, wakisema tasnia ya habari imepoteza chanzo muhimu cha habari ambaye alitoa ushirikiano na kuwa tayari kuelezea masuala ya uchumi kwa majira na katika mazingira yoyote.

Aidha, mwaka jana Profesa Ngowi alizungumza na Nipashe namna ajali za barabarani zinavyogharimu uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Profesa Ibrahimu Lipumba, mtaalamu wa uchumi, aliiambia Nipashe kwamba taifa litamkumbuka kutokana na namna alivyofanikiwa kufikisha hoja zake katika masuala ya uchumi, kupitia maandiko yake kwenye vyombo vya habari na katika ufundishaji.

"Nimepata taarifa asubuhi kwa masikitiko makubwa kifo cha ghafla cha mchambuzi makini, aliyeshiriki mijadala mbalimbali na kuandika makala. Alikuwa bado kijana, tulitarajia kuwa naye mtaalamu muhimu, mtaalamu wa watu. Pigo kubwa kwa taifa na familia, taasisi, chuo," alisema Prof. Lipumba.

Profesa Samwel Wangwe, alisema Prof. Ngowi alikuwa mchumi mahiri aliyejipambanua kwenye masuala ya kiuchumi hususan kwenye sera na ufundishaji.

"Naweza kusema taifa tumepoteza mtu mahiri alikuwa na mchango mkubwa ambao bado ulikuwa unahitajika, Prof. Ngowi alikuwa maeneo mengi kuhusu uchumi utabaini uwapo wake," alisema Prof. Wangwe.

Kadhalika, mshauri na mchambuzi wa masuala ya uchumi, Marko Sillayo, alimwelezea Prof. Ngowi kama mtaalamu aliyejikita kuwaandaa vijana kwenye sekta hiyo, akisema aliweza kuondoa msamiati mgumu wa masuala uchumi ambayo baadhi ya jamii iliamini kwamba ni mambo magumu.

"Tumepoteza mdadavuaji wa uchumi wengi huogopa kuuchambua uchumi, lakini yeye alitumia lugha rahisi kuuelezea. Hata mwalimu huweza kupendwa na wanafunzi kutokana na namna anayotumia mbinu za kufundisha na kuelewa, ndivyo alivyokuwa Prof. Ngowi, taifa limepoteza mtu mahiri, hata sisi tumejifunza kutoka kwake," alisema Sillayo.

Aidha, Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, aliandika kwenye ukurasa wa tweeter: Prof. Honest Ngowi umelala. Hongera kwa kazi nzuri uliyoifanya hapa duniani. Fikra zako nyingi ziko hai kwenye maandishi na sauti, zinaishi. Naye, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliandika katika tweeter: Mara 100 kuwa na akina Ngowi. Mara kadhaa tulitofautiana na Ngowi kuhusu maudhui na mawanda ya makala zake magazetini. Lakini jambo moja kubwa alilofanya ni kuhakikisha anaandika na kuandika. Yeye hakuwa sehemu ya maprofesa wa kuandika page (ukurasa) mmoja kwa mwaka. Alijitofautisha."

**ALITOA TATHMINI YA AJALI**

Mwaka jana alizungumza na mwandishi wa gazeti hili na kueleza namna ajali zinavyodhoofisha uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja kwa watu kupoteza wapendwa wao ambao walikuwa wategemezi wao, watoto kukosa wazazi wa kuendeleza kuwasomesha na kuwahudumia, majeruhi kuugua kwa muda mrefu kulazimu familia kutumia fedha nyingi kuwatibu na wengine kuwa na ulemavu wa kudumu ambao ni gharama kubwa.

Alisema pia nchi inapoteza nguvu kazi na walipa kodi huku akipendekeza maboresho kwenye miundombinu na usimamizi wa sheria ili kuhakikisha usalama wa vyombo vya moto kwa watumiaji wote.

**SHUHUDA ASIMULIA**

Shuhuda wa ajali ya Prof. Ngowi, Josephine Gunda, alisema gari yake ndiyo iliyombeba marehemu kumwahisha Hospitali ya Tumbi na umauti ulimkuta wakiwa njiani.

Gunda ambaye ni Diwani Viti Maalumu Halmashauri ya Kibaha, alisema akiwa njiani kuelekea katika Hospitali ya Mloganzila walikuta ajali katika eneo la Miwaleni, na kwamba walimkuta Prof. Ngowi akiwa ametolewa kwenye gari amelazwa chini.

Shuhuda huyo alisema walipomwona bado anapumua waliamua kumpakiza kwenye gari kumuwahisha hospitalini, lakini walipofika vipimo vya daktari vilionyesha ameshafariki.

"Sisi tulikuwa tunapita tukakuta hiyo ajali tuliposhuka kushuhudia tuliona Prof. Ngowi ametolewa na wamemlaza chini tukaona kama vile amezimia tulipoona bado anapumua tulichukua hatua ya kumkimbiza akapate matibabu ya haraka katika Hospitali ya Tumbi," alisema.

***Imeandikwa na Christina Mwakangale, Salome Kitomari na Julieth Mkikeri (PWANI)**

# Kikosi kazi chategwa kuhusu Katiba Mpya

**Na Sabato Kasika**

BARAZA la Kuu la Uongozi la Chama cha Wananchi (CUF) Taifa, limepinga pendekezo la kikosi kazi kuhusu suala la katiba mpya kushughulikiwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, kwa madai kwamba, hakuna mjumbe aliyependekeza hivyo.

Aliyetoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana ni Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuelezea msimamo wa baraza hilo lililokutana mwishoni mwa wiki.

Mwenyekiti huyo alisema katika mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, uliibuka na mapendekezo zaidi ya 80 likiwamo la uhitaji wa haraka wa katiba mpya.

"Kikosi kazi kilichoundwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji, kilikuwa na kazi ya kuchambua maoni yetu na kisha kuyarejesha kwetu wadau wenyewe, lakini ajabu ni kwamba na chenyewe kinajipa jukumu la kutoa mapendekezo," alisema Prof. Lipumba.

Alisema, baraza hilo linasikitishwa na hatua zilizochukuliwa na kikosi kazi hicho, na kwamba ni vyema serikali na wadau wote wajue CUF na wajumbe wote wa mkutano huo walitamani katiba mpya ipatikane haraka.

Prof. Lipumba alisema, kikosi hicho kilitakiwa kuchambua mapendekezo kwa kuangali yanayofanana na kuyaweka kundi moja na siyo kutoa mapendekezo mengine zaidi ya yale yalipendekezwa na wajumbe wa mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Akiwasilisha mapendekezo kwa Rais Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita, Mwenyekiti wa kikosi kazi, wake Prof. Rwekaza Mukandala, alitaja sababu kadhaa za kupendekeza mchakato wa katiba mpya kuanza baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Prof. Mukandala alitaja baadhi ya sababu kuwa ni uwapo wa haja ya kuainisha dira mpya ya maendeleo ya 2063 itakayotoa mwelekeo wa katiba mpya na suala la kukosekana kwa muda wa kutosha kuanza kutumia katiba mpya ndani ya kalenda ya Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Nyingine ni kutoa fursa kwa marekebisho ya sheria ya uchaguzi na sheria ya vyama vya siasa na haja ya kutoa fursa ya kutosha kufanyia kazi masuala ya muda wa kati ikiwamo kuainisha dira mpya ya maendeleo.

Aidha, alisema kuna changamoto mbili, anazoziona, ikiwamo ya watu wanaosema hakuna haja ya kuwa na katiba mpya na kwamba inaweza kufanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji ya sasa na baadaye, lakini ya pili kuna wale wanaodai kwamba, mchakato wa kupata katiba inayopendekezwa unze haraka.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **24.03.2022** mnatangaziwa hadi **05.04.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili** kuelekea **Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW051Z / ZG2320 KCW052Z / ZG3212 KBQ 628Z / ZE 0941**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita 28.4** |
| **Upana** | - | **Mita 5.0** |
| **Kimo** | - | **Mita 5.6** |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

216769502

# Othman: Sheria ya uchochezi ipitiwe upya

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHERIA ya uchochezi inatoa fursa ya kutumika vibaya na vyombo vinavyosimamia sheria hasa polisi na kwamba wakati umefika wa kuifanyia mapitio ili kulinda uhuru wa kujieleza na wa habari nchini.

Rai hiyo ilitolewa mjini hapo jana na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tatu ya wanasheria kuhusu uhuru wa habari, uhuru wa kujieleza na mashauri ya mahakama yanayohusu uhuru huo.

Othman ambaye ni mwanasheria aliyebobea, amewahi kuwa mwendesha mashtaka mkuu Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Akifungua mafunzo hayo mjini hapo, alisema sheria hiyo kama ilivyo hivi sasa "ina mianya mingi ya kutumika vibaya" na "inaweza kukwaza sio tu uhuru wa habari bali pia uhuru kwa ujumla wake".

Aliwaambia wanasheria na wanahabari kuwa tume za sheria za nchi nyingi zimefanya mapitio makubwa kuhusu mipaka, viini na vitendo mahsusi vinavyosababisha kosa la uchochezi na utafiti uliofanyika unaweza kusaidia Tanzania kudurusu sheria zake.

Othman alisema uzoefu wake kama mwendesha mashtaka umemwaminisha kuwa sheria za uchochezi ni kikwazo kwa uhuru wa habari. "Najua kuwa moja ya vyanzo vikubwa vya habari kwa waandishi ni wanasiasa na viongozi wa kisiasa. Mwandishi anaweza kuingia matatani pale atakaporipoti matamshi halali ya mwanasiasa na vyombo vya sheria vikatafsiri matamshi hayo kama uchochezi," alifafanua.

Alilitaka Baraza la Habari Tanzania (MCT) kama mtetezi wa uhuru wa habari kuanzisha mjadala mpana kuhusu vifungu vya sheria vinavyohusu uchochezi.

"Lililo muhimu ni kwa kila upande kutekeleza wajibu wake na inapobidi kukosoa, kufanyike kwa misingi ya ukweli na haki kwa lengo la kuleta mabadiliko chanya, tukizingatia kwamba sote tunajenga nyumba moja imara, itakayoheshimu haki na uhuru wa habari na kujieleza," alisisitiza Makamu wa Kwanza wa Rais.

Aliishauri pia MCT kuhakikisha kuwa mafunzo hayo yanakuwa endelevu, akiwataka kuandaa mwongozo mahsusi wa ufunguaji mashauri ambao utawasaidia washiriki wa mafunzo hata baada ya kuhitimu, na wale ambao hawakupata fursa hiyo.

Othman alisisitiza kuwa ni muhimu sheria za Tanzania zizingatie Ibara za 18 za katiba zote, ile ya Muungano na ya Zanzibar, ambazo zinazungumzia uhuru wa watu kujieleza.

Aliongeza pia kwamba lazima sheria zikidhi vigezo vya kimataifa ili "kuiweka nchi yetu katika ramani ya kisasa ya uhuru wa habari".

Alitanabahisha kuwa Zanzibar kuna Sheria ya Usajili wa Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu Na. 5 ya mwaka 1988 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 8 ya mwaka 1997, na Sheria ya Tume ya Utangazaji ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2010, lakini "kwa bahati mbaya zote zina changamoto nyingi ambazo zinahitaji marekebisho."

Wabobezi wa sheria nchini wamekuwa wakiongelea sheria hiyo na wakati akifungua maadhimisho ya Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari (EJAT) mwaka 2018, jijini Dar es Salaam, Profesa wa Sheria Issa Shivji alisema sheria za uchochezi zimepitwa na wakati na nchi zinaachana nazo baada ya kubaini kuwa zinakinzana na misingi ya demokrasia.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Baraza la Habari Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC) kupitia International Media Support (IMS).




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungumza wakati akifungua mafunzo kwa wanasheria jijini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vijana kumuenzi Nyerere kwa kutembea siku 6

**Na Richard Makore,** MWANZA

VIJANA 500 kutoka mikoa mbalimbali nchini wanatarajia kutembea kwa miguu kwa siku sita kutokea mkoani Mwanza hadi kijiji cha Butiama, mkoani Mara kwa ajili ya kushiriki kongamano maalum la kuenzi miaka 100 tangu kuzaliwa hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Matembezi hayo yanatarajia kuanza Aprili 7, eneo la Igoma kwenye mnara wa Azimio la Arusha jijini Mwanza na kuhitimishwa Aprili 13, katika kijiji cha Butiama.

Katika matembezi hayo kutakuwa na vituo sita vya kupumzika na kila siku vijana hao watakuwa wanatembea saa 10 kuanzia asubuhi hadi jioni wanapopumzika.

Mratibu wa matembezi hayo, Abdalah Mohammed Ramadhani alisema safari yao itaanza Aprili 7.

Alisema Aprili 6, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, atazindua matembezi hayo na vijana wataanza safari ya kuelekea Butiama.

Wakiondoka watatembea saa 10 na kulala eneo la Nyanguge, wilayani Magu, mkoani Mwanza na Aprili 8 watatoka na kupumzika Magu, siku zote hizo watashiriki shughuli mbalimbali za kijamii zikiwamo upimaji wa virusi vya Ukimwi (VVU) kwa hiari, kuchangia damu na upimaji wa Covid-19.

Alisema Aprili 9, watatoka Magu na kupumzika katika kambi maalum eneo la Nyashimo, Aprili 10, wataingia eneo la Lamadi na kupumzika na sehemu zote watafanya shughuli mbalimbali za kijamii.

Aprili 11, wataanza safari yao hadi wilayani Bunda na Aprili 12 wataingia kijiji cha Kyabakari na kulala kabla ya kuingia Butiama siku inayofuata kwa ajili ya kushiriki kongamano maalum la miaka 100 la kuenzi siku ya kuzaliwa kwa hayati Mwalimu Nyerere.

Ramadhani alisema, vijana wanaotakiwa kushiriki ni wale waliojitolea na wenye uzalendo na kila mshiriki atatakiwa kuchangia Sh. 40,000 kwa ajili ya gharama za tisheti na kofia.

Katika kumbukizi hiyo kutakuwa na maonyesho ya filamu maalum ijulikanayo kama 'Urithi Wetu' ambayo imechezwa na wasanii kutoka Kanda ya Ziwa.

# Wafunguka RPC aliyetamani cheo cha Sirro

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wametoa maoni yao juu ya kauli ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera (RPC), Wankyo Nyigesa, kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan kumteua kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania aliyekuwa (IGP) Simon Sirro bado anaihudumia nafasi hiyo.

Baadhi walisema siyo jambo baya kwa mtu kutamani cheo fulani huku wengine wakisema siyo sawa kutamani nafasi ya juu wakati aliyonayo hajaifanyia kazi ipasavyo.

Mratibu wa Mtandao wa Kutetea Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumo, alisema mtu kutamani cheo cha juu siyo dhambi bali inaweza kutafsiriwa tofauti endapo atatumia njia za hujuma kupata nafasi anayoitamani.

"Siyo vibaya kuomba kuteuliwa, huwenda kuna kitu kakiona kuwa hakiko sawa na kufikiri kuwa endapo atapatiwa nafasi hiyo anaweza kukirekebisha hivyo huo ni ujumbe kwa IGP aliyopo," alisema Olengurumwa.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema misingi ya kiutendaji kazi au cheo cha kuteuliwa hakiombi ila Rais humteua mtu pale atakapoona kuwa anafaa.

"Watu wote hawawezi kuwa nafasi za juu usitamani cheo kikubwa wakati katika nafasi uliyopo bado hujatatua yaliyopo, katika mkoa alipopelekwa kuna mambo mengi ya kipolisi hayapo sawa hivyo tulitegemea angewaambia wanaKagera kuwa huko anakokwenda atafanya nini kutatua changamoto zilizoko," alisema Anna.

Akizungumza jana Kibaha mkoani Pwani wakati wa sherehe za kumuaga baada ya kuhamishwa katika mkoa huo na kupelekwa Kagera RPC Nyigesa, alisema moja ya malengo yake na ndoto zake kubwa ni kuteuliwa kuwa Mkuu wa Polisi nchini (IGP) na anatamani Rais amteue huku akiahidi kuwa atafanya kazi kubwa.

Alibainisha kuwa awali alikuwa anajiandaa kuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Kamishna wa Zanzibar, lakini baada ya nafasi hizo kuchukuliwa sasa anajiandaa kuwa IGP, na aninaamini kwamba Rais Samia anayasikia maombi yake.

"Siku moja tafadhali niteue kuwa IGP, mimi naamini nitafanya makubwa, huwa ninaomba sana Mama (Rais) siku moja aniote tu halafu anitamke tu niwe IGP,

Mimi nitamuomba nifanye miaka mitatu halafu nimwambie Mama mimi nakukabidhi naondoka unaonaje hapo," alisema Nyigesa.

"Binadamu lazima uangalie mbele, natamani kuwa IGP, najua IGP aliyopo Sirro hajafanya makosa anafanya mazuri, lakini mimi nitafanya mazuri zaidi, matarajio yangu ni hayo, unajua binadamu lazima uwe na malengo ya mbele, uwe na ndoto kubwa, huwezi tu kuwa una malengo ya kwamba nitaendelea tu kuwa RPC ...mimi nataka kuwa nafasi za juu, ili nifanye makubwa kwa faida ya Watanzania wengi kuliko wa mkoa mmoja," alisema Nyigesa.

Aliongeza kuwa anaamini siku moja Rais atakapomwona vizuri anaweza kumpa U-IGP na matamanio yake ni kuhudumu katika nafasi hiyo, na alimhakikishia mkuu huyo wa nchi kuwa endapo atamwona anafaa na kumteua atakuwa amepata mtu sahihi kwa wakati sahihi.

TANGAZO


NMB
Karibu yako
Karibu Yako Zaidi!
Huduma za WAKALA
kiulaini, fasta na nafuu
kupitia simu yako tu!
NMB pesa WAKALA
Tshs
Kuwa Wakala
Tsh
OPEN
Ya 1 Tanzania
Pesa Karibu Yako | Kitaani Kwako
Papo Hapo! #NafuuRahisiSalama
Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tawi la NMB lililo karibu yako.
216779602
Vigezo na Masharti kuzingatiwa
www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## WMA zielimishwe kuhusu uhifadhi kipindi cha UVIKO -19

**HIFADHI** ya Jamii ya Burunge, Wildlife Management Area (WMA), iliyoko Tarafa ya Mbugwe, Wilaya ya Babati Vijijini mkoani Manyara, yenye kilomita za mraba 283 inayomilikiwa na vijiji 10, ni moja ya eneo la utalii lililoathiriwa na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 kwa mapato yake kupungua kutokana na uchache wa watalii.

Hifadhi hiyo mali ya vijiji vya Mwada, Sangaiwe, Ngolley, Vilima Vitatu, Kakoi, Minjingu, Olasiti, Maweni, Magara na Manyara ambavyo kwa kutambua umuhimu wa uhifadhi vilitoa maeneo yao na kuunda hifadhi ili kulinda maliasili ya wanyamapori na uoto wa asili.

Eneo hilo limelazimika kuwa WMA kwa sababu kuna mapito ya wanyama maarufu kama Shoroba ya Kwakuchinja ambayo inaunganisha Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na Hifadhi ya Taifa Tarangire, kuwezesha wanyama kuwa salama wanapovuka kutoka eneo moja kwenda jingine.

Ili maliasili hiyo iwe salama ni lazima wananchi wahusike kuitunza kikamilifu, lakini ni lazima wajue faida za kutunza kama ilivyojitokeza kwa Burunge ambako kuna uwekezaji wa hoteli za kitalii, uwindaji na upigaji picha kitalii, shughuli ambazo huingiza mapato.

Katika eneo hilo wawekezaji mbalimbali wamewekeza hoteli za kitalii ikiwamo inayotazama Ziwa Manyara na Ziwa Burunge ambako wanyamapori wa aina mbalimbali husambaa eneo hilo na kuwa kivutuo kwa watalii, huku mapato yakiingia kwa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Halmashauri ya Babati.

Burunge WMA ni kati ya Jumuiya 38 zinazotambulika nchini na kati ya 16 zilizosajiliwa na miongoni mwa nne zinazofanya vizuri kimapato, walianza na makusanyo ya Sh.milioni 300 ambayo yaliongezeka hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 2.2 mwaka 2018/19.

Makusanyo hayo hugawanywa kwa WMA asilimia 65, TAWA asilimia 25 na halmashauri asilimia 10, kwa mwaka waliopata Sh. bilioni 2.2 kila kijiji kilipata Sh. milioni 104 kwa ajili ya shughuli za kipaumbele kwenye eneo lao kwa kadri ya mkubaliano ya wananchi.

Kijiji hicho kwa fedha za utalii wamejenga zahanati ya kisasa na kuweka vifaa tiba, shule ya msingi, ofisi ya kijiji ya kisasa, wametengeneza barabara kwa kiwango cha changarawe na kusomesha wanafunzi wanaofaulu kwenda vyuo vikuu.

Kutokana na UVIKO-19 wageni kutoka nje ya nchi wamepungua na sasa mapato yameporomoka hadi Sh. milioni 400, huku mgawa kwa kila kijiji ukipungua na miradi ya kijamii kusuasua, huku baadhi ya maeneo wakianza kuchangishana.

Miaka ya nyuma kutokana na michango ya kuchangia huduma za kijamii baadhi walikimbia makazi yao kukwepa michango, na sasa baadhi wameanza kujihami.

Hadi sasa WMA imeanza kuongea na wananchi kuendelea kuwa wavumilivu kwa kuwa UVIKO-19 itakwisha na mapato yataendelea kupatikana, lakini kubuni miradi rahisi isiyo ya gharama kubwa ambayo wananchi wataimudu.

WMA hizi zinazotunzwa na wananchi zinahitaji kuelimishwa ili wananchi wasifike mahali wasione faida ya maliasili hiyo, kwa kuwa changamoto ni nyingi ikiwamo mazao kuharibiwa na wanyamapori, watu kujeruhiwa au kuuawa, uharibifu wa mali na ujangili ambao wanafutwa machozi kwa kupata fedha za miradi ya maendeleo.

UVIKO-19 tutaendelea kuishi nayo ni lazima kuzifundisha WMA namna ya kutumia raslimali zilizoko kupata fedha, kuendelea kuvutia watalii kuamini kuwa waneweza kuendelea kutembelea vivutio hivyo na kubaki salama.

Wanyamapori ni rasilimali muhimu ambayo huliingizia taifa fedha za kigeni, inahitaji kutunzwa na jamii ndiyo inahusika moja kwa moja, ili hifadhi hizo ziendelee kuwepo ni lazima wanyama wanapopita kwenye shoroba wawe salama, na kwa wakati huu maeneo haya yanahitaji elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa uhifadhi kwa faida yao na vizazi vijavyo.

Tunaamini kwa kuwa wameshaonja faida ya uhifadhi kwenye miradi ya huduma za kijamii na kwa mtu mmoja mmoja mwanaye kusomeshwa hadi chuo kikuu, wanatambua umuhimu wa maliasili hiyo, wanawajibika moja kwa moja kuhakikisha inakuwa endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

### Muungwana Lazima Nilonge

## Elimu ya vita rushwa ya ngono shuleni isambazwe kote nchini

**RUSHWA** ya ngono imekuwa ikitajwa kushamiri katika shule za msingi, sekondari na vyuo, ikichangia kukwamisha baadhi ya wanafunzi wa kike kutimiza ndoto zao katika elimu wanaponaswa na rushwa hiyo.

Tuhuma za rushwa ya ngono kwa wanafunzi, huwa zinawaangukia madereva wa bodaboda, bajaji, daladala, walimu na hata watu wazima mitaani wanaotumia mbinu mbalimbali kuhakikisha wanawanasa mabinti.

Mfano hai ni pale madereva wanapotumiwa kuwarubuni kwa lifti, ili kuwawahisha shuleni huku walimu wakitumia ahadi za kuwapa majibu ya mitihani, lakini kwa wengine mitaani wakidaiwa kutumia fedha zao kuwanasa.

Hata hivyo, kuna jitihada mbalimbali zinazofanywa na taasisi za serikali zikiwamo Taaisisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kushirikiana na wadau wanaopambana na vitendo hivyo, ili kuhakikisha vinakomeshwa.

Miongoni mwa jitahada hizo imo ya wiki iliyopita ya semina ya walimu walezi wa klabu za kupinga rushwa kwenye shule za msingi na sekondari jijini Dodoma, iliyoandaliwa na TAKUKURU.

Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, katika halfa hiyo anawataka walimu walezi wa klabu za kupinga rushwa kuwajenga wanafunzi uadilifu na uzalendo wa mapambano dhidi ya rushwa wakiwa shuleni.Anataka walimu wasaidie taasisi hiyo kufanikisha elimu ya kuzuia rushwa inawafikia wanafunzi kwa ufasaha, huku akiipongeza TAKUKURU kuanzisha klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi na sekondari mkoani humo.

Kimsingi, tatizo la rushwa ya ngono kwa wanafunzi limeenea nchi nzima, hivyo kwa mtazamo wangu ni kwamba kama mikoa mingine itaiga mfano ulioanzishwa na TAKUKURU Mkoa wa Dodoma.

Ninaamini kwamba, iwapo mfano huo utaigwa itakuwa ni rahisi shule zote nchini kuwa na klabu hizo za kupinga rushwa na ngono na kuwafanya wanafunzi kuwa na uelewa wa kutosha wa kupambana na rushwa hiyo.

Inawezekana wapo baadhi ya wanafunzi hawajui madhara ya ngono, wengine wanaweza kuwa wanajua lakini wanashindwa kujisimamia, hivyo kuwapo semina, klabu zao shuleni vinaweza kuwabadilisha wakawa makini.

TAKUKURU wakifika kila nchini na kutoa semina kuhusu madhara ya rushwa ya ngono, hatua hiyo inaweza kuongeza kasi ya uelewa kwa wanafunzi wanaosomea katika mazingira hatarishi.

Ikumbukwe kuwa wapo baadhi ya wanafunzi wanaotembea umbali mrefu kwenda shule na kurudi nyingine, wengine wanaishi katika nyumba za kupanga mitaani kutokana na shule kutokuwa na mabweni.

Mazingira hayo ni hatarishi kwa mwanafunzi wa kike, kwani ndiyo ambayo huwaingiza kwenye vishawishi vya kupewa lifti ili wawahi shule au kurubuniwa kwa ahadi za kulipiwa kodi huko wanakopanga mitaani.

Kuwapo semina za kila mara zinazotolewa na TAKUKURU kwa kila shule nchini, kutasaidia kudhibiti rushwa ya ngono hata kugundulika na kupungua haraka, kwani wahusika watakuwa wameelewa madhara yake na jinsi ya kuikwepa.

Vivyo hivyo, nao TAKUKURU wakitoa semina kwa wanafunzi kila mara na kuwaelekeza wapi pa kushtaki wanapokutana na rushwa hizo, itawarahisishia kukataa unyonge wa lifti, kupewa majibu ya mitihani au fedha.

Nionavyo, si vibaya kuendelea kuongeza walimu wa kike wengi shuleni na kuwapandisha vyeo, ili viwafanye angalau wawepo ni watu wawili wa juu wanaotoa uamuzi katika shule husika na kufuatilia kwa ufasaha mienendo ya wanafunzi wa kike, wakiwapa semina za malezi kuwaondoa katika hatari ya mahusiano.

Njia hizo zinaweza kusaidia kuwafanya wanafunzi ambao wapo katika klabu za kupambana na rushwa ya ngono kuwa mabalozi watakaosaidia kuwaimarisha wenzao katika vita hiyo inayohatarisha maendeleo yao kielimu.

Ni hatua inayotokana na ukweli kwamba, klabu hizo za shuleni zinawasaidia wanafunzi kubadilishana mawazo na kupeana uzoefu na mikakati ya kupambana na rushwa hiyo nyumbani, mitaani, njiani na shuleni.

# Wanaume watajwa matukio ukatili wa kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWANASAIKOLOJIA Edward Mwendamseke, amesema takwimu na kasi ya matukio ya ukatili wa kijinsia nchini, vimekuwa vikiongezeka kila uchao, kwa sababu idadi kubwa ya wanaume hawana mahali pa kupumulia matatizo yao wanayopitia katika maisha, ukilinganisha na wanawake.

Akizungumza juzi katika kampeni ya kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu, inayoendeshwa na Shirika la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE CDO katika Kata ya Njiapanda, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo ulioko mkoani Kilimanjaro, Mwendamseke alisema:

“Mwanamke anaongea maneno 24,000 mpaka 26,000 kwa siku, kwa sababu yeye anatafuta mara nyingi njia za kuondoa hali ya kihisia anayoisikia ndani yake, ambayo inasababisha yeye kuwa na matatizo mbalimbali. Wakati mwanaume anazungumza maneno 6,000 mpaka 7,000 kwa saa 24. Uwezo wa mwanaume kueleza matatizo yake anayopitia ni mdogo sana, ukilinganisha na uwezo wa mwanamke kujieleza kwenye matatizo anayopitia.

“Kwa mfano, ukiangalia huu mfumo umetengenezwa pia katika mfumo wa malezi, unaweza kuwa shahidi kwamba namna unavyomlea mtoto wa kiume, ni tofauti na tunavyomlea mtoto wa kike. Mtoto wa kiume tunamlea kama ni mtu ambaye ni mlinzi, ni mtu ambaye ni mkakamavu, ni mtu ambaye hatakiwi kuonekana ananung’unika au kulalamika.

Kwa hiyo huwa inamnyima mtoto wa kiume, kuwa na tabia ya kueleza matatizo aliyonayo, na ndio maana unaweza ukakuta sio tu kuongea, hata kulia mtoto wa kiume akilia ni tofauti na tunavyomchukulia, tofauti na akilia mtoto wa kike.”

Alipoulizwa ni kwa nini mwanamke anazungumza maneno mengi zaidi, mwanasaikolojia huyo alisema, mwanamke ana marafiki wengi, ana watu anaowatumia kwenye jamii kueleza matatizo anayopitia, ikiwamo kutafuta msaada.

“Hiyo kuongea maneno mengi ni sehemu ya yeye kupumua au kuelezea hisia ambazo anakuwa anapitia katika maisha yake ya kawaida.

“Ndio maana hata ukienda kwenye nyumba za ibada, mfano kanisani utakuta wanawake pamoja na kwamba idadi yao ni kubwa; lakini bado kwenye hayo maeneo wanakuwa wengi sana, kwa sababu wao wanatumia hiyo njia kama eneo muhimu sana ya kukabiliana na matatizo wanayopitia kwenye maisha yao ya kawaida.”

Kwa mujibu wa Mwendamseke, ambaye ni Mwenyekiti na Mwanzilishi wa Shirika la Youth Empowerment & Psycotherapy Organization, (YEPAO), ukiangalia wanaume wao njia zao ni njia butu, kwa sababu wao wanakimbilia kwenye matumizi ya vilevi kama pombe.

“Utakuta wamejazana kwenye baa, utakuta wanaangalia mpira na vitu vingine ambavyo ni burudani.

“Vitu hivyo kwa wanaume vinasaidia sehemu ndogo sana, ukilinganisha na maneno ambayo walipaswa kuyazungumza ili kutatua tatizo. Na ndio maana tunasema moja ya vitu vinavyochangia sana wanaume kufa mapema ni kushindwa kueleza changamoto walizonazo ili waweze kuepukana na msongo wa mawazo.”



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Kampuni ya Mafuta ya Puma Tanzania, Dk. Seleman Majige (kushoto), akimkabidhi tuzo mmoja wa mawakala wa vituo vya mafuta vya kampuni hiyo kutoka mkoani Arusha, Hussein Sajan, baada ya kushinda tuzo ya mwaka 2021/2022, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wateja Halopesa kuibuka na bodaboda, fedha

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Halotel Tanzania kupitia mfumo wake wa huduma za kifedha jana imezindua rasmi promosheni ya Shinda na Halopesa ambayo inawapa wateja wake fursa ya kujishindia zawadi za fedha taslimu pamoja na bodaboda.

Akiongea katika uzinduzi huo, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa HaloPesa, Magesa Wandwi alisema; “tunafurahi wakati wote kuwa katika tasnia hii ya utoaji wa huduma za kifedha kidigitali, huduma ambazo zinawapa wateja wetu na umma wa Watanzania kwa ujumla fursa ya kufanya miamala kwa njia ya simu ikiwa ni pamoja na kutuma pesa kutoka HaloPesa kwenda HaloPesa na mitandao mingine, kwenda benki, kununua muda wa maongezi na vifurushi, kulipia bili na malipo mbalimbali, huduma za serikali, kutoa fedha kwa mawakala wetu na katika ATM.”

Alisema wamekuja na promosheni hiyo ili kuendelea kutia chachu na hamasa kwa wateja na Watanzania wote kuendelea kutumia huduma za kifedha ikiwa ni katika malengo na ajenda ya serikali kuwafanya wananchi wengi zaidi kutumia mifumo rasmi ya kifedha.

Alisema promosheni hiyo itaendeshwa kwa muda wa wiki nane na maalumu kwa wateja wa HaloPesa. Jumla ya wateja 72 watajishindia zawadi, wateja 64 watajishindia zawadi za fedha taslimu zitakazotolewa kila siku kwa kipindi chote cha wiki nane, wapo watakaojishindia Sh. 50,000 hadi 100,000 kwa kila siku.

Vile vile, wateja wanane watajishindia bodaboda mpya moja kila wiki kwa kipindi cha wiki nane.

“Tunawakaribisha na kuwahimiza wateja wetu wote na wale ambao hawajaanza kutumia huduma ya HaloPesa kuchangamkia promosheni hii kwa kufanya miamala mingi wawezavyo,” alisema.


## TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA

### TAARIFA YA UPANUZI WA MASHIMO YA GENA NA GOKONA YALIYO KATIKA MGODI WA DHAHABU WA NORTH MARA, WILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA

Mradi pendekezwa wa upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona (Mradi) upo ndani ya Wilaya ya Tarime katika Mkoa wa Mara nchini Tanzania. Mradi pendekezwa unamilikiwa na Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM) ambayo ni kampuni ya utafutaji na uchimbaji madini inayomilikiwa na kampuni ya Twiga Corporation, iliyoundwa kwa ubia kati ya Barrick (84%) na Serikali ya Tanzania kwa (16%). Eneo la Mradi liko chini ya Leseni ya Uchimbaji Maalum (SML 17/96). Mradi pendekezwa unazigusa kata nne ambazo ni Nyamwaga, Nyarokoba, Kibasuka na Kemambo pamoja na sehemu za vijiji vitano: Komarera, Genkuru, Msege, Kewanja na Nyakunguru.

Upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona ni muendelezo wa shughuli za uchimbaji pamoja na faida za kiuchumi zitokanazo na shughuli hizo za uchimbaji. Kwa miaka mingi, NMGM imekua ikiendeleza tafiti katika eneo hilo ambazo zimeonyesha uwepo wa mashapo yaliyopo kwenye mashimo hayo.

Ili kutekeleza Mradi pendekezwa, Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) itafanyika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira ya mwaka 2005 na marekebisho yake ya mwaka 2018 pamoja na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

NMGM imeziteua kampuni za Digby Wells Environmental na PAULSAM Geo-Engineering Limited kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Utafiti huo utachunguza athari chanya na hasi kwenye mazingira na jamii zitakazotumika kuunda Mpango wa Usimamizi wa Mazingira kwenye utekelezaji wa Mradi.

Kwa kuzingatia utaratibu, usajili pamoja na uwasilishwaji wa taarifa za awali za mradi kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) unaendelea kama sehemu ya TAM. Tangazo hili linawakaribisha watu wote wenye nia, ushauri au maarifa kuhusu athari zozote ama za kimazingira au kijamii zinazohusiana na mradi huu kuwasilisha mawazo yao kwa kupitia anuani zifuatazo:

| Mdhibiti | Muwekezaji | Wataalamu washauri elekezi |
|---|---|---|
| Mkurugenzi Mkuu<br>Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC),<br>S.L.P. 63154, Regent Estate,<br>Dar es Salaam, Tanzania.<br>Simu: +255 22 2774889<br>Barua pepe: dg@nemc.or.tz | Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM)S.L.P. 422<br>Tarime<br>Tanzania<br>Faksi: 255282621903<br>barua pepe: apolinary.lyambiko@barrick.com | PAULSAM Geo-Engineering Company Limited,<br>Ghorofa ya 07 , Faykat Tower Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam, Tanzania.<br>S.L.P. 70812<br>Simu/Faksi: +255 755561188<br>Barua pepe: piliseleman@gmail.com |
| | | ESD Advisory Ltd T/A Digby Environmental<br>Madai Crescent, Plot 151, Ada Estate, Dar es Salaam.<br>Jamii:+255717087482<br>Barua pepe: Deogratius.lorri@digbywells.com |

**Ushirikishwaji wa wadau utafanyika kama sehemu ya mchakato wa TAM ambapo habari zaidi zinazohusiana na mradi zitawasilishwa.**

216778302

# Shamrashamra zaanza mkutano wa CCM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI zikiwa zimebaki siku tatu kufanyika kwa Mkutano Mkuu maalum wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) jijini Dodoma, nyumba za kulala wageni zimeanza kuadimika kutokana na idadi kubwa ya watu kuanza kuwasili kwa ajili ya shughuli hiyo.

Pamoja idadi kubwa ya watu kuanza kuwasili jijini hapa, pia barabara za jiji la Dodoma zimepambwa bendera za chama hicho katika maeneo mbalimbali.

Nipashe jana ilifanya uchunguzi katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma na kubaini kuwa upatikanaji wa vyumba katika hoteli pamoja na nyumba za kulala wageni umekuwa wa shida, tofauti na wiki moja iliyopita.

Nipashe lilipita katika maeneo ya Mji mpya na maeneo mengine ya nje kidogo ya Jiji la Dodoma na kushuhudia nyumba nyingi za kulala wageni zikiwa zimebandikwa kibao cha vyumba vimejaa.


Hali hiyo imekuwa kero kwa baadhi ya wageni ambao wamekuwa wakiwasali jijini hapa kwa ajili ya shughuli nyingine za kikazi tofauti na mkutano huo wa CCM.

"Sisi tumeingia Dodoma juzi, lakini shida tuliyoipata ni vyumba vya kulala maeneo mengi tuliyokwenda yamejaa na leo hii nikimaliza kazi hii sijui kama nitapata chumba kwa ajili ya kulala," alisema mmoja wa watu ambao wamekutana na adha hiyo.

Mwakilishi wa Taasisi ya Sekta Binafasi Tanzania (TPSF) mkoa wa Dodoma, Ringo Ilingo, alisema mkutano wa CCM ni kioo cha kuutambulisha mkoa wa Dodoma, hivyo jitihada zinahitajika kuwekeza kwenye huduma ya malazi.

"Halmashauri za mkoa wa Dodoma zinatakiwa kutumia fursa hii kutenga maeneo ya uwekezaji wa hotel pamoja na nyumba za kulala wageni zenye ubora hivyo yawepo maeneo tena kwa bei nafuu ili kuvutia wawekezaji," alisema.

"Maeneo mengi ya kulala wageni bado hayana ubora kwani hoteli nyingi bado ni nyumba za chini taasisi za fedha zinatakiwa kutoka mikopo kwa watu kuwekeza maeneo ya huduma hizi za malazi, hivi sasa Dodoma inakwenda kuwa mji wa kitalii kutokana na kuanza kwa ujenzi wa uwanja wa kisasa wa ndege hivyo lazima kuanza kujipanga sasa," alisema Ringo.




Meneja wa Wateja Maalum wa Tigo, Mary Ruta (kulia), akabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni mbili kwa Majeshi Salim, aliyeibuka mmoja wa washindi wa kwanza 20 wa promosheni inayoendelea ya 'Pesa Mwaa Mwii na Tigo Pesa', jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB Pesa Wakala sasa yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua huduma maalumu ya kuweka na kutoa pesa kirahisi kupitia wakala watakao tumia simu zao za mkononi tu.

Huduma hiyo ya NMB Pesa Wakala ilizinduliwa jijini Dar es Salaam, ikilenga kusogeza karibu zaidi huduma za kifedha kwa wananchi, pamoja na kutoa fursa za ajira kwa Watanzania, lengo likiwa kuongeza idadi ya mawakala kutoka 11,000 wa sasa, hadi 100,000 miaka mitano ijayo.

Akizungumza wakati wa kuzindua huduma hiyo, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alivitaja vigezo vya mtu kuomba uwakala wa NMB Pesa Wakala kuwa ni pamoja na Leseni ya Biashara, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) na simu ya mkononi ya aina yoyote (smartphone au kitochi).

"Tunaahidi kwamba kupitia teknolojia hii mpya na ya aina yake, mfanyabiashara mwenye vigezo vilivyotajwa, ataweza kuomba na kuwa 'activated' ndani ya saa 48 tu toka atakapoomba matawini kwetu kote nchini, naye ataweza kuhudumia wateja wake.

"NMB ni vinara wa huduma suluhishi zinazowafanya Watanzania wafurahie huduma za kibenki. Tunafanya hivyo kwa sababu sisi ni benki inayotegemewa na Watanzania wote, ndio maana tunayo furaha kuzindua NMB Pesa Wakala ili kuharakisha maendeleo ya Sekta ya Fedha nchini," alibainisha Mponzi.

Aliongeza kuwa, huduma hiyo itaenda sambamba na ile ya Vituo vya Mauzo (PoS), na kwamba tofauti huitaji kupata mashine maalumu na sasa mteja anaweza kutoa huduma hii kupitia simu yake ya mkononi tu, bila kuhangaika kupata mashine za PoS ambazo zinatumia kadi.

"Tunaamini NMB Pesa Wakala itaharakisha kusambaza mawakala wengi zaidi wa kusogeza huduma kwa jamii, lakini itakuwa fursa ya kuongeza ajira miongoni mwa Watanzania. Tunajisikia fahari kuja na suluhishi hili na tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha tunaendelea kuwa vinara wa huduma za kifedha nchini," alisisitiza Mponzi.

# Taboa yalia na sheria kandamizi barabarani

**Na Richard Makore,** MWANZA

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi yaendayo Mikoani (TABOA), kimeomba serikali kuondoa sheria kandamizi za usalama barabarani, ili kuweka mazingira bora na rafiki ya kufanya biashara.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku mbili baada ya serikali kutangaza mabasi yaendayo mikoani kuanza kutumia mfumo mpya wa kielektroniki katika kukatisha tiketi kuanzia Apili 1, mwaka huu.

Kadhalika, TABOA imetangaza kiama kwa "vishoka" ifikapo Aprili 1, mwaka huu baada ya kuanza kutumika mfumo wa ukatishaji tiketi kielektroniki.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Mwanza, Katibu Mkuu wa TABOA mkoani Mwanza, Anwari Seif, alisema ifikapo tarehe hiyo wamiliki wa mabasi hawatawahitaji 'vishoka' kwa kuwa kila kitu kitakuwa katika mfumo rasmi wa kielektroniki katika ukusanyaji mapato.

Alisema baada ya mfumo huo kuanza watakuwa na watu maalum ambao wamesajiliwa kwa ajili ya kukatisha tiketi hizo na hesabu zao zitakuwa zinafanyiwa hesabu na Mamlaka ya Mapato (TRA), ili walipe kodi.

Alisema watu hao ambao wanajulikana pia kama ''wapiga debe'', wamekuwa tatizo katika vituo vya mabasi kwa kuwa wanachukua fedha nyingi za wamiliki wa mabasi.

Alitoa mfano kwamba mpiga debe ama kishoka anaweza kupokea Sh. 40,000 kutoka kwa abiria kama nauli ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini yeye anapeleka Sh. 30,000 kwa mmiliki wa basi.

Alisema baada ya mfumo huo kuanza watu wakaokatisha tiketi ni wale waliosajiliwa kisheria, wanaotambuliwa na wamiliki wa mabasi pamoja na TABOA.

''Kwa sasa gharama za uendeshaji wa mabasi haya zipo juu, mafuta yamepanda, kodi zipo juu na vipuri navyo vimepanda bei, sasa akitokea tena mtu akaondoka na fedha nyingine ambazo hazipo katika utaratibu inakuwa shida kidogo,'' alisema.

Kuhusu kasoro mbalimbali walizokuwa wakilalamikia kabla kwa kaunza mfumo huo, Seif alisema nyingi zimefanyiwa kazi na serikali, ingawa bado wanahitaji kuondolewa sheria kandamizi.

Alisema wamekubaliana na serikali kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki katika kukatisha tiketi, na kwamba wameiomba kurekebisha sheria kandamizi kabla ya Julai mwaka huu.

Alisema mfumo huo utaanza kwa majaribio mwezi ujao, lakini utaanza rasmi Julai mosi, mwaka huu na kwamba kabla ya kufikia kipindi hicho, kuna mambo yanatakiwa kuwekwa sawa.

Alitoa mfano wa sheria kandamizi, Seif alisema ni kondakta akikutwa barabarani hajatoa tiketi za kielektroniki kwa abiria anayepigwa faini ya Sh. milioni tatu ni mmiliki wa basi na siyo yeye.

Aidha, alisema hawajakubaliana kati ya serikali na wao wamiliki namna ya uendeshaji wa mfumo huo pamoja na kikokotoo cha mahesabu yanayopatikana kwa kila basi.

Hata hivyo, alisema wameahidiwa na kamishna wa kodi za ndani wa TRA kwamba kasoro hizo zitarekebishwa kabla ya kufikia Julai mosi, mwaka huu, mfumo huo utakapoanza rasmi.

## Kampeni usafi mazingira yaiva Wilaya ya Handeni

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA kuelekea Siku ya Usafi wa Mazingira Duniani Septemba, Asasi ya Usafi na Uhifadhi wa Mazingira (RUVU) ya mkoani Tanga kwa kushirikiana na Asasi ya Nipe Fagio zilifanya usafi kijiji cha Segera, mkoani Tanga Machi 26, mwaka huu.

Mwenyekiti wa asasi hiyo, Sharifu Chakachaka, alisema usafi huo ni mwanzo wa programu ya kufanya uhamasishaji wa kuweka mazingira safi kwa mkoa wa Tanga ili ikifika siku ya usafi duniani mkoa huo uwe msafi.

"Programu hii tumeiita 'Pre cleanup' kwa maana ya kwamba maandalizi ya usafi kabla ya siku ya usafi duniani, lengo ni kuweka mazingira safi polepole badala ya kusubiri kufanya hivyo kwa siku moja," alisema Sharifu.

Naye Mratibu wa Siku ya Usafi Duniani Wilaya ya Handeni, Abdallah Lundo, alisema kuwa usafi huo utafanyika kila baada ya miezi mitatu mpaka itakapofika siku ya usafi duniani.

"Tumeanza leo Machi 26, tunategemea kurudi tena hapa Juni 26 na mwisho ni hiyo siku ya usafi duniani Septemba 17, mwaka huu, tumeanzia Wilaya ya Korogwe sasa tunaelekea Handeni lengo ni mkoa mzima wa Tanga upate hamasa hii," alisema Lundo.

Aliongeza kuwa usafi huo unafanyika kwenye maeneo ambayo hayamilikiwi na mtu yeyote ambayo takataka zinazagaa bila kuondolewa kama vile kwenye vituo vya mabasi, sokoni na pembezoni mwa barabara.

"Lengo pia ni kuangalia ni aina gani ya taka hizi zinazagaa sana mitaani na kupeleka habari kwenye mamlaka husika, mfano leo tumepata mifuko 50 ya takataka sasa tunachambua tukiona nyingi ni za kampuni fulani tunatoa taarifa kwenye mamlaka husika," alifafanua. Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Segera, Majuto Yussufu, alisema kuwa amefurahishwa na mwitikio wa wanakijiji katika suala hilo na kuwa litakuwa linafanyika kila mwezi.

"Tunashukuru asasi ya RUVU kuja kutuelimisha kuhusu umuhimu wa kuweka mazingira safi na pia mwitikio wa watu umenipa moyo wa kuendeleza utamaduni hii kila mwezi," alisema.

Bakari Samsechu, mwanakijiji wa eneo hilo alisema amefurahishwa na jinsi walivyopendezesha eneo hilo kwa kuwa hapo mwanzo halikuwa na mwonekano mzuri.

"Kabla ya usafi hili eneo lilikuwa na taswira mbaya, takataka zilijaa kando ya barabara, nyingi ni chupa za plastiki zinazotupwa na abiria wa mabasi ya mikoani, sasa hivi limependeza sana, napendekeza suala hili lifanyike kila mwezi," alisema.

# ACT yajiweka kando rufani ya makada CHADEMA waliofungwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

UONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo mkoani Lindi, umesitisha dhamira ya kukata rufani kwa ajili ya kuwasaidia kutoka gerezani wanachama wanne wa CHADEMA Kata ya Majengo, Halmashauri ya Mtama kwa kile ulichodai kuondoa malumbano na wenzao.

Tamko la kusitisha dhamira hiyo lilitolewa na mwenyekiti wake wa mkoa, Rashidi Mchinjita, alipokuwa anazungumza na Nipashe mjini Lindi.

Wanachama hao walihukumiwa adhabu ya kifungo cha miaka minane kila mmoja na Mahakama ya Mkoa wa Lindi, Februari 18, mwaka huu kwa kosa la kuharibu mali na kujeruhi watu wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Wanachama hao ni Rajabu Hassani, Moshi Hamisi, Dadi Shayo na Hamisi Maleje, wakazi wa Kata ya Majengo katika Halmashauri ya Mtama.

Alisema kwa sasa uongozi wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Lindi umeamua kusitisha mpango huo, kwa kile alichokieleza kuepusha malumbano na CHADEMA kwa kuwa viongozi wao wameonyesha dhamira ya kushughulikia suala hilo.

Tulikuwa na dhamira ya dhati ya kukata rufani kuwasaidia, lakini wenzetu wameonyesha dhamira ya kukata rufani, hivyo tunawaachia," alisema Mchinjita.

Pia mwenyekiti huyo alisema ACT-Wazalendo na CHADEMA ni wamoja katika kushughulikia mambo mbalimbali, hivyo asingependa kuwapo malumbano kati ya vyama hivyo kuwapo upendo, umoja na mshikamano kama ndugu.

Alieleza iwapo viongozi wa CHADEMA watahitaji msaada kutoka kwao, wapo tayari kushirikiana nao katika kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa.

"CHADEMA sio wagomvi wetu, ni ndugu zetu, mgomvi wetu hapa ni Chama cha Mapinduzi (CCM), alisema Mchinjita.

Februari 19, mwaka huu, kwenye mkutano wa ACT-Wazalendo uliofanyika mjini Lindi, Mchinjita alitangaza nia ya kukata rufani kupinga hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa huo dhidi ya makada hao wa CHADEMA.

Hata hivyo, siku chache baadaye, uongozi wa kukata rufani CHADEMA ulianza kushughulikia rufani ya kupinga hukumu hiyo dhidi ya makada wake.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja (watatu kushoto), akitoa maelezo ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Makongo hadi Bagamoyo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge Hesabu za Serikali walipotembelea utekelezaji wa miradi hiyo jijini Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali rufani yataka elimu lugha ya alama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HOSPITALI ya Rufani mkoani Shinyanga, imeomba kupatiwa elimu ya lugha za alama kwa watumishi wake, ili kurahisisha utoaji huduma za matibabu kwa watu wenye ulemavu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. John Luzila, alitoa ombi hilo juzi wakati akizungumza na Nipashe, juu ya adha ambazo wanakumbana nazo na namna ya kuzitatua wanapopata wagonjwa wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) na kuongea (bubu).

Alisema wanapopata wagonjwa wenye ulemavu, hupata tabu ya kuchukua taarifa zao pamoja na maelezo ya kujua wanasumbuliwa na tatizo gani, na kuomba kama kuna uwezekano wa taasisi yoyote ambayo inajihusisha na elimu maalum, ifike kwenye hospitali hiyo na kutoa elimu ya lugha za alama kwa watumishi.

"Tunapata shida sana ya kutoa matibabu kwa watu wenye ulemavu wanapofika kupatiwa matibabu katika hospitali hii, lakini watumishi wetu huwa wanajitahidi kuelewana nao kwa kutumia ishara na kuwapatia tiba," alisema Dk. Luzila.

"Ninachokiomba kwa watu hawa wenye ulemavu, wanapokuja kupatiwa matibabu waje na wakalimani wao pamoja na vielelezo ya utambulisho wao ili iwe rahisi kupata maelezo yao na kuwapatia tiba stahiki," aliongeza.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii katika Hospitali hiyo, Prisla Mushi, ambaye ana husika kwenye ofisi ya mapokezi ya wagonjwa, alisema wanapopata wagonjwa wenye ulemavu huwa wanajitahidi kupata taarifa zao kwa ishara na kuelewana nao, na wale ambao hushindwa kuelewana, hutafuta mbinu ya kuwapatia matibabu.

"Mimi na nesi mmoja yupo kitengo cha uzalishaji ndiyo kidogo tunajaribu kuwasiliana na wagonjwa wenye ulemavu kwa ishara na endapo tukishindwa kuelewana, walemavu wengine huwa wakali na kuanza kufanya fujo," alisema Mushi.

Aidha, alisema kuna kipindi kati ya mwaka 2013 au 2014 kuna baadhi ya watumishi hospitalini hapo walipatiwa elimu ya kuzijua lugha za alama, lakini hawapo, na kuomba elimu hiyo itolewe tena ili waifahamu na kuwa rahisi kwao kutoa huduma stahiki ya matibabu kwa watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) mkoani Shinyanga, Richard Mpongo, aliiomba serikali kupeleka wataalamu wa kutafsiri lugha za alama kwenye taasisi zote za serikali, ili wasije wakakosa huduma kwa sababu ya kushindwa kuelewana.

# Alivyouawa kikatili kwa madai wivu wa mapenzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKULIMA wa Kijiji cha Hingawali, Wilaya ya Lindi mkoani hapo, Imamu Halfani Kigogo (38), ameuawa kwa kucharangwa mapanga na wananchi wanaojiita wenye hasira kali, chanzo kikidhaniwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Taarifa zilizothibitishwa na ndugu wa marehemu na Jeshi la Polisi, zinaeleza Kigogo amepatwa na umauti Machi 17, mwaka huu jioni.

Kwa mujibu wa shangazi wa marehemu, Pimageni Machemba, ndugu yake aliuawa kwa kukatwa mapanga maeneo mbalimbali ya mwili wake, ikiwamo kichwani na mbavuni, kisha kuutelekeza mwili kando ya njia za waenda kwa miguu.

"Taarifa ni ya kweli, mpwa wangu ameuawa kikatili kwa kukatwa mapanga kichwani pamoja na kuvunjwa mbavu," alithibitisha, huku machozi yakimtiririka.

Amesema familia haijafahamu chanzo cha mauaji hayo, na kuwa wanamwachia Mungu na Jeshi la Polisi waendelee kufanya kazi yao ya kuwasaka wahusika wa mauaji hayo.

Hata hivyo taarifa kutoka kwa baadhi ya wanaomfahamu marehemu (majina tunayahifadhi) zinadai kuwa Kigogo aliuawa kutokana na wivu wa mapenzi alipokwenda nyumbani kwa mpenzi wake.

Wamedai Kigogo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke (jina limehifadhiwa) anayeishi kijijini hapo na alipotaka kuingia ndani vijana waliokuwa nje ya nyumba hiyo walimpigia kelele za mwizi na kuanza kumshambulia.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutokea kwa mauaji ya mwanakijiji huyo na kueleza kuwa jeshi hilo linaendelea na upelelezi kuwabaini waliohusika ili sheria ichukuwe mkondo wake.



Mkuu wa Idara ya Hisabati, Jinsia na Sayansi ya Jamii wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Dk. Laurencia Massawe (kulia), akikabidhi samani za viti vilivyotolewa msaada na chuo hicho kwa Shule ya Sekondari ya Ulongoni, Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam. Katikati anayepokea ni Ofisa Elimu (Taaluma - Dar es Salaam), Nyange Mtoro na kushoto ni mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo, Ramadhani Sawaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIT yasaidia madawati, viti shuleni Dar

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimetoa msaada wa samani mbalimbali zikiwamo meza 19 na viti 2 vyenye thamani ya milioni 2.6/- kwa Shule ya Sekondari Ulongoni iliyoko wilayani Ilala mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi msaada huo kwa niaba ya Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, Mkuu wa Idara ya Hisabati, Jinsia na Sayansi ya Jamii, Dk. Laurencia Massawe, alisema msaada huo ni sehemu ya uwajibikaji wa kijamii kwa taasisi hiyo ambapo kusaidia elimu ni miongoni mwa vipaumbele vyake.

"Novemba mwaka jana, Mkuu wetu wa Chuo, Prof. Mganilwa alialikwa na Shule ya Sekondari Ulongoni wakati wa mahafali ya kidato cha nne ambapo aliombwa kusaidia shule hiyo samani za ofisi ya walimu," alisema.

Alisema baada ya kupokea maombi hayo NIT iliona ni muhimu kusaidia shule hiyo kwa samani za walimu ili kuwafanya waweze kufanya kazi zao za ufundishaji kwa ufanisi na na kuwasaidia wanafunzi kufanya vizuri zaidi kwenye masomo yao.

"Ndiyo kwa sababu hii, leo tumekuja kukabidhi samani zenye thamani ya shilingi milioni 2.6 kusaidia shule hii iweze kupunguza baadhi ya changamoto zinazowakabili," aliongeza.

Anasisitiza: "Pia tunatoa msaada huu kwa kuthamini umuhimu wa elimu. Ni matamanio yetu kuona walimu wanafanya kazi katika mazingira yanayovutia kufundisha."

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Sikitiko Salehe, aliushukuru uongozi wa NIT kwa msaada huo, na kuyataka mashirika mengine kuiga mfano unaoonyeshwa.

Alibainisha kuwa mwaka jana uongozi wa Shule ya Sekondari Ulongoni ulipeleka maombi yao kwa mashirika mbalimbali ya umma na binafsi katika kupata msaada wa samani za walimu kwa shule yao na NIT imeitikia ombi lao.

"Tunaishukuru NIT kwa kujibu ombi letu na leo tumepokea jumla ya meza 19 na viti 2 ambavyo vingesaidia kuziba pengo la uhaba," alisema.

Salehe alisema kuwa msaada huo umekuja wakati mwafaka na kuahidi vazi lake kuwa tayari kutunza samani hizo. Alisema mbali na uhaba wa samani, shule hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo ukosefu wa uzio wa ukuta, madarasa ambayo sasa yamekuwa chakavu, vyoo na uhaba wa madawati.

## Vituo afya vyaagizwa utoaji wa huduma za TB

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, ametoa maelekezo kwa vituo vya afya kutoa huduma ya kifua kikuu kwa wananchi na kwamba serikali ipo tayari kutoa dawa katika vituo hivyo.

Dk. Kamba alitoa maelekezo hayo juzi, baada ya kubainika kuwa vituo vingi vya binafsi havitoi huduma ya kifua kikuu, huku kukiwa na takwimu za kuhudumia asilimia 40 ya wagonjwa wote nchini.

"Nitoe wito kwa vituo vyote vya mkoa wa Pwani vitoe huduma za kifua kikuu kuanzia sasa, serikali ipo tayari kutoa dawa kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya kifua kikuu kwa urahisi," alisema Dk. Kamba.

Aliwataka wananchi wanapoona dalili za ugonjwa huo kuwasiliana na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ili waweze kupata tiba sahihi kutokana na taarifa ya wagonjwa wengi wa kifua kikuu kuishia kwenye tiba mbadala na maduka ya dawa muhimu.

Mratibu wa kifua kikuu na ukoma mkoa wa Pwani, Dk. Aden Mpangile, alisema mkoa wa Pwani umefikia zaidi ya asilimia 90 ya ugunduzi wa wagonjwa wa kifua kikuu kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo.

Dk. Mpangile alisema mwaka 2018 wagonjwa 2,919 waligundulika, 2019 (3,024), mwaka 2020 (2,851) na 2021 (2,671) ambapo katika ugunduzi huo pia asilimia 15 ya watoto waligundulika, lakini pia wagonjwa wa kifua kikuu sugu kutoka tisa hadi 24 waligundulika baada ya kupata mashine za kisasa za uchunguzi.

Kwa Mujibu wa Dk. Mpangile, bado wana vikwazo katika ugunduzi wa wagonjwa wa kifua kikuu ndani ya mkoa huo ambavyo ni pamoja na vituo vichache vya binafsi ambavyo vinatoa huduma za afya, huku vituo vingi vya uchunguzi kuwa mbali, hivyo wananchi kutopata huduma kwa urahisi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 29, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**KUTOKA MRADI ELIMU JUMUISHI SHY...**
Magumu ya walimu wasio na stadi madarasani kwa wenye ulemavu



Ukurasa 12

**Wanafunzi mkondo wa PCM waonyesha maajabu kuwapiku wahandisi kompyuta**

ELIMU

NA DK. CAESAR JJINGO, KAMPALA

# Ufundishaji Kiswahili Uganda unavyoleta mkanganyiko ndani

## ■Kitendawili cha saa chawatoa jasho

JE, walimu nchini Uganda
wafundishe Kiswahili kama
walivyofundishwa, wafuate
vitabu au wafundishe ka
waonavyo wenyewe?

Kwa makusudi, anwani ya mak
hii nimeiandika na kuiwekea alama
kuuliza mwishoni. Sababu kuu ya k
fanya anwani kuwa swali, ni kuta
kuwashawishi wasomaji kujiuli
maswali mbalimbali yatakayoibu
kabla ya kuyasoma, bali hata wak
na baada ya kusoma makala haya.

Kwa haraka, kwa upande wan
naona tayari anwani inaony
sha kuwa na majibu matatu
Ninaamini bado kuna majibu ibu
mbalimbali yanayoweza kufikiriw
zaidi kwa wasomaji.

Kwa kifupi, ni swali linalotoka
na mvutano wa kimawazo ulio
tokeza mnamo Machi 19 mwa
huu, kwenye jamvi la mtanda
wa 'Whatsapp' lijulikanalo kam
CHAKITAU (Chama cha Kiswah
cha Taifa - Uganda).

Jamvi hilo linawaunganish
wadau mbalimbali wa Kisw
hili nchini Uganda, wakiwam
walimu wa Kiswahili wa nga
mbalimbali.

Jamvini humo, tarehe hiy
majira ya saa sita mchana, kul
kuwapo mjadala mwingine w
kitaaluma uliokuwa ukiendo
lea, ndipo mmoja wa walim
kwenye jamvi hilo akalet
picha ya saa ya ukutani.

Kwenye picha hiyo, mshal
mfupi ulikuwa kwenye tan
na mshale mrefu ukaw
kwenye 12. Mwalimu huy
alitaka asaidiwe kuambiw



TENDERS
OVER 150 DEALS IN KOLE, PRIDE MICROFINANCE...

GOVT REGISTERS, CLEARS 2,000 NGOS, LIST ON P4

New Vision

Thursday, November 14, 2019 Vol.034 No.228 Price: USH 2,000 (KSH 107, TZSH 1

KISWAHILI COMPULSORY FOR O'LEVEL P5

LUMUMBA STARTS PEACE TALKS AMONG KAMPALA NRM LEADERS
In a bid to defuse tension among Kampala National Resistance Movement (NRM) leaders, the party secretary general, Justine Kasule Lumumba, has initiated peace talks. A source who attended the first meeting said the discussion centred around the newly appointed mobilisers, **writes David Lumu. P4**

PARLIAMENT
Fraud: Kadaga blows whistle
Parliament's Speaker Rebecca Kadaga yesterday told MPs that sh24b meant for a bridge connecting Kayunga and Kamuli districts had been 'chewed', writes **Moses Walubiri. Page 7**

ST READ 1
UPDF in Rwenzori
The Uganda People's Defence Forces

Gazeti la nchini Uganda, likiwa na habari sasa Kiswahili ni somo la lazima. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**

ile picha ya saa ilikuwa inaonyesha
saa ngapi kwa Kiswahili.

Baadhi ya wadau (akiwamo
mwandishi wa makala hii)
waliandika kuwa ni saa 5 kamili
na wengine (akiwamo mwalimu
aliyeleta picha ya saa ukutani)
wakaandika saa 11 kamili.

Hapo ndipo vuta nikuvute ilipoan-
zia. Je, wewe unadhani ile mishale
a saa ilikuwa inaonyesha saa ngapi?
Hivyo, baada ya kutofikia mwafaka,
liyeileta ile picha ya saa jamvini
kaandika kwenye jamvi yeye ata-
afundisha wanafunzi wake ajuavyo
wenyewe.

Ni kweli nchini Uganda, Kiswahili sio
ti ya lugha asilia za nchi hiyo. Hivyo,
ipishana kimawazo kwenye masuala
mila, desturi na tamaduni za Waswa-
li ni kitu cha kawaida ila sio kwenye
mbo dogo' kama la kusoma saa.

Ingawa kuna yanayochangia wengi
shindwe kusoma saa, suala la walimu
aliotufundisha na vitabu tulivyovisoma
vya msingi zaidi kuzingatiwa.

Masuala ya walimu na vitabu vya Kiswa-
li nchini Uganda si mageni, bali ni ya
historia. Ikumbukwe, ingawa Kiswahili
lifika Uganda miaka ya 1840 kikitokea
venye mwambao wa Afrika Mashariki,
amishionari wa Kikristo walikiingiza
smi kwenye mifumo ya elimu ya nchi hiyo
iaka ya 1920.

Hivyo, tangu hapo Kiswahili kimekuwa
kikumbwa na misukosuko hasa kutoka kwa
atetezi wa lugha asilia za nchi hiyo.
Hivyo, kimekumbwa na matatizo ya kiuta-

INAENDELEA UK.13

TEKNOLOJIA


NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Wanafunzi mkondo wa PCM waonyesha maajabu kuwapiku wahandisi kompyuta

- Wabuni programu zinazotumika shuleni
- Roboti walizotengeneza zaibua gumzo
- Lugha wanavyofafanua 'mainjinia watupu'



Peniel Nshimba (kushoto) akielezea jambo kuhusu roboti maalum kwa ajili ya kupima udongo akiwa na mwenzake, Johnson Nyimbo (kulia).



Roboti iliyobuniwa na Peniel na Johnson.

UNAPOZUNGUMZIA kipaji ni talanta mtu anayozaliwa nayo, pindi mtu anapoingia kwa undani zao la kipaji ni ubunifu, kwa nchi zilizoendelea wabunifu wana nembo kubwa na kuwafanya waishi.

Wazo la kubuni kitu fulani ni msaada kwenye jamii na kupunguza vikwazo, kuokoa muda na kuondokana na urasimu ikiwa hatua muhimu katika nchi zinazoendelea, mfano unaopaswa kuchukua hatua katika nchi zinazoendelea.

Zao hilo linaendana na ubunifu ulioonyeshwa na baadhi ya wanafunzi wa sekondari Loyola, iliyoko Mabibo mkoani Dar es Salaam, hasa katika mbinu rahisi ya ama kuandikisha au kusajili taarifa za mtaka huduma. Huwa inaleta mwanga na inapokubalika kidigitali inaweka kumbukumbu mara moja na kuokoa muda.

Chrispin Lubava (17), ni mwanafunzi wa kidato cha tano anayesoma mkondo wa PCM. Amebuni programu wezeshi itakayomsaidia mwalimu kuweka kumbukumbu za taarifa za mwanafunzi, bila kubaki kutegemea kuandika katika makaratasi na kutunza kwenye mafaili.

Chrispin, anaiambia Nipashe kuwa programu hiyo ameipa jina la 'data base management', alipokuwa kwenye maonyesho ya ubunifu wa wanafunzi shuleni hapo, ikiwa ni sehemu ya shughuli za siku ya uzinduzi wa bweni la wasichana, lililozinduliwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe.

Chrispin anasema, alitafakari kwa muda mrefu namna ya kuingiza taarifa za mwanafunzi kwa kutumia analogia, ndipo alipokuja na wazo hilo. Anaeleza: "Changamoto ya kutunza mafaili, kwanza yanachukua 'space' (nafasi ) kubwa.

"Ukiwa na programu hii, itahitajika kompyuta tu moja, eneo dogo ambalo ndani itakusanya taarifa nyingi hadi mamilioni, ni namna unavyo 'i-command' (ielekeza).Kuna kipindi mwanafunzi mmoja kwenye orodha ya wanaofanya mtihani taarifa zake hazikuwekwa kwenye mafaili, yaani hakusajiliwa.

"Lakini 'app' hii kama mwalimu ana orodha ya wanafunzi 45 darasani, namba moja ikikosa jina la mwanafunzi ataona 'gap' (pengo) ila katika faili ngumu kubaini," anaongeza mwanafunzi huyo wa mchepuo wa sayansi.

Anasema pia programu hiyo inafaa, iwapo ikitokea mto kwenye taasisi fulani, mafaili yakiungua una maana taarifa zote zimepotea.

"Mimi kwa sababu ndio niliyebuni, nina uwezo wa kuwa na 'back up' ya kutunza taarifa hizi mahali pengine, iwapo kompyuta itapotea. Programu hii inaweza kutumika katika vituo vya afya, hospitali na taasisi nyingine," anaeleza.

Anatumia mfano unaofanana kwamba katika vituo vya afya, mtoa huduma anaweza kumwandikisha mteja (mgonjwa) kwa kuingiza taarifa zake kwenye kompyuta na zikasoma moja kwa moja kwa daktari, ambaye atakwenda kumuona; ni hali inayotumika sasa katika hospitali kubwa nyingi nchini.

"Ukifika vituo vidogo vya afya, wagonjwa huandika taarifa zao katika daftari. Ni maeneo machache ambayo tayari yana kompyuta kwa sasa nchini kuandika taarifa za mteja. Pia ninaweza kutengeneza tovuti.

"Nilianza kuonyesha ubunifu wangu kupitia maonyesho ya kila mwaka shuleni, kuna 'clubs' za vipaji. Desemba mwaka jana wakati wa likizo nilikamilisha kuandaa, kisha nikafanikiwa wazo la programu huonyesha haya ndio nimekuja na kitu hiki. Ila haijaanza kutumika bado," anaeleza mwanafunzi huyo, anayetaja katika siku zijazo kuwa 'software engineer' (mhandisi kompyuta).

Anaisifu kuwa programu yenye uwezo wa kuongeza idadi ya mahitaji kulingana na mtumiaji anavyotaka na anatoa wito kwa jamii kutumia vipaji vya wabunifu na kuviendeleza.

**WAWILI WABUNI**

Wasomi mwengine, Peniel Nshimba (17) na Johnson Nyimbo (18) kutoka shule hiyo, pia wote wakiwa kidato cha tano wanasomea 'PCM', vipaji hadi ubunifu wao umewafanya kutambulika Kimataifa na kupata tuzo kimataifa na kuwaacha mbali washiriki kutoka mabara mengine.

Peniel anaiambia Nipashe kwamba mwaka 2018 wakiwa kidato cha pili walitunukiwa nishani ya 'bronze' kutokana na kubuni roboti inayomsaidia mkulima au mwendelezaji matumizi kwenye ardhi kubaini kiwango cha maji katika udongo na 'acidity level' (kiwango cha kemikali) ya udongo.

Kijana anayetaja ndoto yake kuwa mhandisi wa sayansi kompyuta atakayejiajiri katika taasisi yake ya kiteknolojia itakayoasisi vyombo mbalimbali vya kompyuta na kusaidia jamii, anaeleza: "Tuzo tuliyopata... ilihusu mradi unaoitwa AGRIBOT. Huyu ni robot ambaye anamwezesha mkulima kupata taarifa kuhusu mazao yake shambani kutumia simu yake.

"Hii ni muhimu, kwa sababu mazao mbalimbali hukua katika udongo wenye aina fulani ya madini katika kiwango fulani. Iwapo roboti huyu atatumika hili itainua wingi wa mazao katika mavuno na kuinua uchumi wa mkulima."

Pia wanafunzi hao, nao wamebuni programu iitwayo 'student report system', ambayo humsaidia mwalimu kuweka taarifa za kila mwanafunzi.

"Ilitokea mwalimu wetu wa Kemia aliwahi kupoteza matokeo ya maksi (alama) za wanafunzi. Kwa hiyo alihitaji 'app' ambayo anaweza kuingiza maksi za wanafunzi na kutoa repoti moja kwa moja, bila kutumia nguvu yoyote.

"App hii ina usalama wa 'password'. Mwalimu pekee anaweza kuingia katika mfumo huu. Pia mwanafunzi au mzazi anaweza kuangalia matokeo hayo bila kusubiri kufika shuleni kuchukua matokeo hayo, atatumia tu simu au 'laptop' yake.

"Changamoto katika kutengeneza hii 'system' ilikuwapo katika kuhakikisha usalama katika mfumo huu kwenye intaneti. Ila data haziwezi kupotea, maana kuna 'backup' huwa inakua 'created' " anasema Peniel, huku mwenziwe Johnson, anadokeza ndoto yake kuwa mhandisi kompyuta.



Chrispin Lubuva, akielezea kuhusu programu ya 'data management' kwenye kompyuta, kwa washiriki waliofika kwenye maonyesho ya vipaji vya wanafunzi Shule ya Sekondari Loyola, mkoani Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Ufundishaji Kiswahili Uganda unavyoleta mkanganyiko ndani

INATOKA UK.11

wala, kisera na hata utekelezaji. Hatimaye mwaka 1952, Kiswahili kilifutwa kwenye mifumo ya elimu nchini humo, kutokana na sababu hasa zisizo za kielemi na kilibaki kuwa lugha ya kufundishia mafunzo ya jeshi na shule mafunzo ya polisi.

Nchini Uganda, Kiswahili kilianza kusikika tena kwenye mifumo ya elimu mwishoni mwa miaka 1980. Hivyo, uhaba wa walimu na vitabu ulijitokeza mara moja.

Kwa mfano, baadhi ya wazawa wa Uganda na raia wengine kutoka Tanzania, Kenya na Zaire (sasa DRC) walitumia fursa hiyo kuanza kufundisha Kiswahili nchini humo, ingawa wote hawakuwa walimu waliohitimu kufundisha Kiswahili, hasa kama lugha ya kigeni.

Walikuwa na viwango mbalimbali vya matumizi. Vilevile, 'walimu' hao na baadhi ya wajasiriamali nchini Uganda walitunga na kuandika 'vitabu' na vijitabu vya Kiswahili viweze kutumika shuleni.

Ikimbukwe, ingawa Sera ya Lugha ya Elimu ya 1992 ilitamka Kiswahili kifundishwe kama somo la lazima kuanzia shule za msingi hadi za sekondari, haikutaja ni lahaja ipi ya Kiswahili ifuatwe na walimu shuleni.

Ukimya wa sera ulivipa 'viswahili' mbalimbali kushamiri kwenye ngazi tofauti za elimu nchini Uganda. Viswahili hivi mara nyingi vilitegemea eneo alilotoka au alilokulia mwalimu wa Kiswahili wa shule au chuo husika.

Hadi hivi leo, matamko mbalimbali ya serikali hayapo bayana juu ya lahaja ipi ya Kiswahili ifundishwe kwenye mifumo ya elimu ya nchi hiyo.

Hivyo, vitabu hasa kutoka nchini Kenya na Tanzania vinaendelea kumiminika nchini humo ingawa pia idadi ya waandishi wa Kiswahili wazawa wa Uganda inaongezeka kila kukicha.

Taswira ijitokezayo hapa ni kwamba, nchini Uganda, kwa muda mrefu, masuala ya ufundishaji wa Kiswahili ni kama soko huria lilivyo ambapo mtu yeyote mwenye umilisi wowote ule wa lugha hii aliweza kuwa mwalimu na kuingia darasani kufundisha.

Kwa mantiki hiyo, naweza nikawa sahihi pia nikisema kwamba walimu wengi wa Kiswahili nchini Uganda hatukupata misingi madhubuti ya lugha hii, jambo ambalo linaweza likawa ni sehemu ya chanzo cha misuguano ya kimawazo baina yetu hata kwa 'kitu kidogo' kama kusoma saa!

Isitoshe, kuna kasumba nyingine inayojitokeza ambayo tumejijengea sisi wenyewe kwamba, tulitayarishwa vya kutosha na walimu wetu, hivyo hakuna haja au budi kujifunza kutoka kwa wenzetu ambao sio wazawa wa mwambao wa Afrika Mashariki.


Kasumba hiyo inaakisi ile ambayo bado inawakunisha vichwa wataalamu wengi dunia wa lugha za kigeni kama kilivyo Kiswahili nchini Uganda.

Wataalamu hao bado wanajiuliza, je, kuna haja ya walimu wasio wazawa kufundisha lugha za kigeni wakati walimu wazawa na wabobevu wa lugha hizo wapo?

Swali kama hili linaweza kuoanishwa na ule mtazamo 'hasi' wa uandishi wa vitabu vya lugha za kigeni na wasio wazawa wa lugha hizo.

Mitazamo mbalimbali kama huo hapo juu na maswali kemkemu yaliyokujia ukiwa unasoma makala haya yanaturudisha pale pale kwenye swali letu kuu ambalo pia ndiyo anwani ya makala haya; Je, walimu nchini Uganda wafundishe Kiswahili kama walivyofundishwa, wafuate vitabu au wafundishe kama waonavyo wenyewe?

• ***Dk. Caesar Jjingo; ni Mhadhiri wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda ana anapatikana kwa anwani: caesarial@gmail.com***




Ramani inayoinyesha kiwango cha Kiswahili kinavyotumika kwenye ukanda mbalimbali nma kiwango chake.




Hafla katika Chuo Kikuu cha Makerere, inayohusu taaluma ya lugha Kiswahili. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

**KUTOKA MRADI ELIMU JUMUISHI...**

# Magumu ya walimu wasio na stadi madarasani kwa wenye ulemavu

- Wanena: Tunataabika, ila huruma tu
- Mkoa wakiri pengo, waomba msaada
- Ngazi ya wizara yaahidi kutenda jambo



Mkurugenzi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Julius Migeha anayeshughulikia Elimu Maalum, (wa pili kutoka kulia) akikata utepe kuzindua Mradi wa Elimu Jumuishi, katika Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga na Misungwi kwa wanafunzi wenye ulemavu. Wa pili kushoto, ni Mkurugenzi wa Shirika la Sense International Naomi Lugoe, (kushoto), Mkurugenzi wa Shirika la Add International Rose Tesha na kulia ni Ofisa Mratibu Mwandamizi wa Elimu Jumuishi kutoka TAMISEMI, PIPeter Ndomondo. **PICHA: MARCO MADUHU.**

SHULE nchini zinazofundisha wanafunzi mchanganyiko, wenye ulemavu, pia wenye afya sawia, zinakabiliwa na upungufu wa walimu wenye stadi za kuwafundisha na kuwachanganya kwenye darasa moja.

Walimu wa kawaida wasio na taaluma ya elimu maalum, wanapoingia darasani, hupata shida kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu.

Upungufu huo wa walimu maalum katika Shule Jumuishi za Shinyanga umedumu muda mrefu, sasa inashuhudia ufumbuzi, baada ya kuzinduliwa mradi wa elimu jumuishi utakaofundisha walimu wa kawaida kuzijua lugha za alama, hata kupunguza tatizo hilo la upungufu wa walimu maalum.

**ELIMU MKOA**

Meneja wa Mradi wa Elimu Jumuishi, Menance Mhombwe, anasema wamedhamiria kuboresha mazingira rafiki ya wanafunzi wenye ulemavu, ili wapate elimu bora sawa na wenzao katika shule hizo jumuishi.

Anasema, wanafunzi wenye ulemavu wamekuwa wakipunjwa fursa ya kupata elimu bora, kutokana na kuwapo na upungufu wa walimu maalum katika shule hizo, sasa wao wamekuja na ufumbuzi wa tatizo hilo, kwa kuwafundisha walimu wa kawaida lugha za alama.

"Mradi wetu huu wa elimu jumuishi tunautekeleza katika shule 47 ambazo zipo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga na Misungwi mkoani Mwanza na utadumu ndani ya miaka minne (2022-2024)," anasema Mhombwe.

"Kazi ambazo tutakuwa tukitekeleza kwenye mradi huu, ni uboreshaji wa mazingira rafiki ya wanafunzi wenye ulemavu kupata elimu bora katika shule jumuishi, kwa kuanza kutatua tatizo la upungufu wa walimu maalum.

"Walimu wa kawaida watafundishwa lugha za alama, na kuanza kufundisha, pia wanafunzi wenye ulemavu," anaongeza Mhombwe.

Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako, anasema upungufu wa walimu shuleni unasababishwa na wanafunzi kutofundishwa ufanisi na anabainisha mkoa wao Shinyanga, unakabiliwa na upungufu wa walimu 5,447 wa shule za msingi.

> "Inafika kipindi unachoka kabisa kufundisha, lakini ukiangalia hawa watoto wanahitaji msaada wetu ili watimize ndoto zao. Inabidi ujikaze tu hivyo hivyo kuwa fundisha na iliwafikie malengo yao," anasema Makambajeki.

Ofisa Elimu Maalum Manispaa ya Shinyanga, Edward Mdagata, anasema serikali bado inaendelea na jitihada za kutatua changamoto za upungufu wa walimu katika shule hiyo ya Msingi Buhangija.

Anasema, kwa sasa ameomba walimu sita waliosomea taaluma maalum wanaofundisha shule za kawaida katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wakafundishe katika shule hiyo ya Buhangija Jumuishi.

**KUTOKA WIZARANI**

Ofisa Elimu Maalum Mwandamizi kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Seleman Chamshama, anataja takwimu za upungufu wa walimu maalum nchini ni asilimia 40.

Anabainisha: "Serikali hatupo nyuma kutatua tatizo hili la upungufu wa walimu wenye mahitaji maalum. Tumeshatoa mafunzo ya vitendo kazini kwa walimu wa shule za msingi wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili (usonji) na viziwi, ili kuzijua lugha za alama kwa ufasaha na kufundisha wanafunzi hao vizuri."

Chamshama anafafanua, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wameshaongeza vyuo vinne vinavyotoa elimu maalum na hivi karibuni vitaanza kudahili wanachuo, ili kuongeza idadi ya walimu wanaosomea elimu maalum, ili kupunguza tatizo la upungufu wa walimu hao.

Mkurugenzi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Julius Migeha, anakiri kuwapo upungufu huo, akifafanua: "Suala hili la kufundisha walimu kozi fupi ya elimu maalum nimelipenda sana.

"Linaenda kupunguza tatizo la upungufu wa walimu maalum katika shule jumuishi, sababu watafundisha wanafunzi wa kawaida na wenye ulemavu."

**WAHUSIKA SHULENI**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi, katika Manispaa ya Shinyanga, Fatuma Jilala, anafafanua kuna jumla ya walimu 19 na kati yao wenye taaluma husika wako 10, akiwa na hitaji la walimu 14.

Anaeleza, wamekuwa wakiomba kupatiwa walimu wenye taaluma maalum, kwa sababu wanafunzi wenye mahitaji hayo wanapaswa kufundishwa kwa stadi za hali ya juu ili waelewe masomo yao, hivyo hakupaswi kuwapo upungufu wa walimu.

"Tunaomba serikali itupatie walimu wenye taaluma maalum ili tuendelee kufanya vizuri kitaaluma, sababu shule inapokuwa na upungufu wa walimu hawa, tunapata shida sana katika ufundishaji kulingana na hali zao," anasema Jilala.

Agnes Makambajeki, ni mwalimu mwenye taaluma maalum anayefundisha katika Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi, naye anakiri tatizo la upungufu wa walimu maalum linawashinikiza wafanya wafanye kazi ya ziada ya kuelewesha kundi linginelo wenye ulamavu.

"Inafika kipindi unachoka kabisa kufundisha, lakini ukiangalia hawa watoto wanahitaji msaada wetu ili watimize ndoto zao. Inabidi ujikaze tu hivyo hivyo kuwa fundisha na iliwafikie malengo yao," anasema Makambajeki.

Martha Mabula, ni mwanafunzi mwenye ulemavu anayesoma darasa la tano katika shule hiyo ya Buhangija, anasema upungufu wa walimu ni changamoto kwao kielimu, kutokana na kushindwa kufundishwa kwa ufanisi.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema ameomba kibali kwa Rais kuajiri walimu 7,000 ili kupunguza upungufu wa walimu ulioko kwa shule za msingi na sekondari nchini.

Anasema awali Rais Samia alishatoa kibali cha kuajiri walimu 6,949, walimu hao walishaajiriwa na tayari wapo kwenye vituo vya kazi wakiendelea kufundisha.





## Sh. bilioni 2.5 kukamilisha soko la wazi la machinga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi wa soko la wazi la machinga jijini Dodoma lenye uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 4,000.

Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na machinga wa Mkoa wa Dodoma baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa mradi huo.

Alisema ili kufanikisha ujenzi wa mradi huo kukamilika kwa wakati, Rais Samia Suluhu Hassan, ameidhinisha fedha hizo ili kupatia eneo la uhakika la kufanyia biashara zao wafanyabiashara hao.

"Mradi huu utawasaidia kupanda juu kimapato, lakini ni eneo lenye usalama kwa ajili ya biashara zenu, hivyo hata taasisi za kifedha zinaweza kuwapatia mikopo kwa ajili ya kukuza mitaji yenu kwa kuwa mpo katika eneo rasmi sasa," alisisitiza Nchemba.

Alisema ili mradi huo usikwame, Rais ametoa kiasi hicho cha fedha ili kutimiza malengo ambayo walikuwa wamejiwekea ya kuwapanga machinga katika maeneo rasmi.

"Aliagiza fedha zitolewe bila kuchelewa hivyo nawaalika timu ya mkoa kuja ofisini na mchanganuo wao wa fedha zitakavyotumika na baada ya mradi huu kukalimilika atakuja mwenyewe kushuhudia," alisema.

Mwigulu, alisema dira ya Rais ni kuwezesha makundi mbalimbali ili kujikwamua kiuchumi na kuondokana na manyanyaso waliyokuwa wakikabiliana nayo na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alimshukuru Rais Samia kwa kuidhinisha fedha hizo ili kuhakikisha machinga wanafanya shughuli zao kwenye maeneo rasmi.

"Tunamshukuru sana Rais kwa kiasi hiki cha fedha ambacho kinakwenda kutoa majibu kwa machinga wetu ambao walikuwa wakipata shida kwa muda mrefu kwa kukosa eneo rasmi kwa ajili ya kufanya biashara zao," alisema.

Pia alisema mradi huo utakapokamilika unatarajiwa kuhudumia wajasiriamali wadogo zaidi ya 4,000.

"Eneo hili ni kwa ajili ya wajasiriamali wadogo ambao tayari tumeshawasajili na kuwahakiki, lakini tumeshaomba kibali kwa TAMISEMI, ili kupata zile fedha za asilimia 10 ya mapato ya ndani kujenda mradi mwingine kama huu njia ya Dar es Saalam," alisema.

Mwenyekiti wa machinga Mkoa wa Dodoma, Bruno Mponzi, alisema kukamilika kwa mradi huo kutawaondolea adha nyingi walizokuwa wakizipata ikiwamo mvua na jua.

"Sisi machinga mradi huu tunausubiri kwa hamu sana kwa kuwa unakwenda kujibu kero zetu ambazo tumekabiliana nazo kwa muda mrefu, lakini utatuwezesha kuaminika na taasisi za fedha kupata mikopo kwa ajili ya mitaji," alisisitiza Mponzi.

# Waziri ataka jengo mpigachapa mkuu kujengwa kwa kiwango

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Balozi Dk. Pindi Chana, amemtaka mkandarasi wa ujenzi wa majengo ya ofisi ya mpigachapa mkuu wa serikali kujengwa kwa viwango vinavyotakiwa. Waziri Pindi aliyasema hayo jana kwenye hafla ya kukabidhi eneo la ujenzi kwa mkandarasi wa ujenzi wa jengo hilo, jijini hapo.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Waziri Mkuu imeidhinishiwa fedha za maendeleo ya ndani Sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa majengo hayo.

Waziri Pindi alisema ujenzi huo unapaswa kukamilika katika kipindi cha miezi 12.

"Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa awamu kutokana na upatikanaji wa fedha, hivyo mwaka wa fedha 2021/22 ujenzi utakaofanyika ni ujenzi wa jengo la kiwanda ambapo gharama ni Sh. bilioni 2.29, na gharama za mshauri elekezi Sh. milioni 389.5 gharama hizi zitajumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT)," alisema.

Aliagiza ujenzi huo uzingatie ubora na viwango kwa mujibu wa mkataba.

"Nimejulishwa kuwa muda wa maandalizi ya kuanza kazi ni wiki mbili kuanzia Machi 25, mwaka huu, kuanza rasmi Aprili 8, mwaka huu na kukamilika mradi ni Machi 7, mwaka 2023," alisema.

Naye mkandarasi ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Hainani International Limited kutoka China, Ding Wu, alisema kuwa atahakikisha Watanzania wanapata ajira badala ya kuwajaza raia wa kigeni.

"Tutahakikisha fedha iliyotolewa na serikali tunamaliza ujenzi huu kabla ya wakati kwa miezi kumi badala ya miezi kumi na mbili tuliyopewa," alisema.



Wadau wa hifadhi na utunzaji wa mazingira kutoka Taasisi ya kifedha ya Fanikiwa, kwa kushirikiana na wakazi wa mtaa wa Zepsa pamoja wanafunzi wa Shule ya Msingi Zepsa wakiwa wamebeba miti kwa ajili ya kuipanda maeneo ya mitaa mbalimbali Kata ya Hombolo Makulu jijini Dodoma, juzi.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wadau mazingira waombwa kutoa elimu mabadiliko tabianchi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WADAU wa mazingira wameombwa kutoa elimu ya mabadiliko ya tabianchi kwa jamii ili ijiepushe na uharibifu wa mazingira.

Mkurugenzi Mtendaji wa Human Originality and Environmental Care Foundation (HUDEFO), Sara Pima, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wakazi wa mtaa wa Zepsa jijini hapo baada ya kukabidhi miche ya miti ya kivuli na matunda kwa ajili ya kuipanda kwenye eneo la zahanati na Shule ya Msingi Zepsa, ikiwa ni sehemu ya sera mpya ya taifa ya mazingira.

Alisema kuna umuhimu wa kutoa elimu hiyo kwa wananchi ili kuondokana na uharibifu huo.

Aliwahimiza wananchi kuwa na tabia ya kupanda na kutunza miti ili kudhibiti uharibifu wa mazingira.

"Kila mmoja abebe ajenda hii ya kupenda kupanda na kuitunza miti iwe ni jukumu lenu badala ya kuiachia serikali na wadau wa mazingira," alisema.

Aidha, aliwahamasisha wanafunzi wa shule za msingi, kuendelea na kampeni iliyoko ya 'Soma na Mti' iliyozinduliwa hivi karibuni inayolenga kupanda miti zaidi ya milioni 14 hapa nchini.

Naye Ofisa Rasilimali watu kampuni ya kifedha Fanikiwa Microfinance, Elizabeth Kapya, aliziomba taasisi za kifedha kuwekeza faida yao kwenye upandaji na utuzaji wa miti vijijini.

Aliomba taasisi hizo kwa kushirikiana na wadau wa mazingira kutoa elimu itakayo wahamasisha wananchi kuwekeza miti ili iwe sehemu ya kujikwamua kiuchumi kupitia miti hiyo.

Kwa upande wake, Ofisa Misitu Msaidizi Jiji la Dodoma, Collin Opiyo, alisema bado kuna uvunaji miti holela bila utaratibu kwa kuchoma mkaa, kilimo na ukataji kuni.

Alisema kutokana na matatizo hayo kuna ulazima wa kuelimisha jamii ili kuhifadhi misitu na Dodoma kuendelea kuifanya kuwa ya kijani.





# Mbeya yakabidhiwa msaada vifaa utunzaji kumbukumbu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la German Corporation for International Development (GIZ), limekabidhi msaada wa vifaa vya TEHAMA, vyenye thamani ya Sh. milioni 597 kwa Mkoa wa Mbeya ili kusaidia utunzaji wa kumbukumbu za utoaji huduma za matibabu katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mbeya, Kyela, Chunya, Rungwe na Kituo cha Afya cha Ipinda.

Akikabidhi vifaa hivyo mwishoni mwa wiki, Meneja Programu anayeshughulikia masuala ya afya, Kai Straehler, alisema Shirika la GIZ linafanya kazi mikoa miwili, Mbeya na Tanga kwa kuzisaidia hospitali na vituo vya afya kuunganishwa na mifumo ya mtandao na mifumo mengine ili kurahisisha mawasiliano na kutunza kumbukumbu.

Alisema vifaa hivyo vimesaidia kuongeza ufanisi wa kazi katika hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati na sasa mgonjwa anaweza kuzipata taarifa zake kwa muda mfupi ikilinganishwa na awali, kumbukumbu zilikuwa zinatunzwa kwa njia ya maandishi.

"Tunafurahi kuona matokeo chanya ya mradi huu wa utoaji vifaa vya TEHAMA ambavyo vimesaidia kuunganisha mifumo ya hospitali zenu kwa sasa wagonjwa wanaotibiwa wanapata taarifa zao ndani ya muda mfupi haya ni mafanikio ya kujivunia jambo la muhimu ni kuomba utunzaji wa vifaa hivi ili viendelee kuwasaidia wagonjwa na kurahisisha mawasiliano," alisema Straehler.

Pia Sh. bilioni 1.1 zimetolewa na GIZ kwa mkoa wa Mbeya na Hospitali ya Rufani ya Mbeya ilipatiwa Sh. milioni 116.8, Hospitali ya Rungwe Sh. milioni 160, Kyela Sh. milioni 134, Chunya Sh. milioni 122 na Kituo cha Afya cha Ipinda Sh. milioni 61.

Alifafanua kuwa kwa Mkoa wa Tanga, Hospitali ya Rufani ya Mkoa ilipatiwaSh. milioni 139, Hospitali ya Wilaya ya Handeni Sh. milioni 115, Korogwe Sh. milioni 125, Lushoto Sh. milioni 119 na Hospitali ya Wilaya ya Tanga Sh. milioni 89.

Alisema madhumuni ya Shirika la GIZ ni kuona huduma za afya zinaboreshwa nchini kwa kuhakikisha mifumo ya TEHAMA, vifaa tiba pamoja na afya ya mama na mtoto inazidi kuimarika.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya mikoa yote miwili, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Abeli Asilia, alisema katika halmashauri nne za Mkoa wa Mbeya zilizonufaika na mradi huo pia vituo vinane vimepata fedha za kuunganishwa na mifumo ya TEHAMA na intaneti.

"Shirika la GIZ wametoa Sh. milioni 597 kwa Mkoa wa Mbeya na Sh. milioni 589 kwa Mkoa wa Tanga, misaada hii mara mbili cha muhimu ni kuandaa mpango kazi wa namna ya utunzaji wa vifaa hivyo kwa kuhakikisha baada ya kipindi fulani kunatolewa taarifa ya maendeleo ya vifaa hivyo," alisema Dk. Asilia.

"Nawaagiza viongozi wa hospitali kutoa taarifa ya kila mwezi kuhusu maendeleo ya vifaa hivi vilivyotolewa, hii itasaidia kuongeza umakini wa kutunza," aliongeza Dk. Asilia.

Alilishukuru shirika hilo kwa kuendelea kutoa elimu ya afya ya uzazi ambayo inalenga kuhakikisha huduma za mama na mtoto zinatolewa inavyotakiwa na kuwaelimisha kinamama namna bora ya kuhudumia ujauzito ili kuepukana na vifo vitokanavyo na uzazi.

Ofisa TEHAMA Mkoa wa Mbeya, Frank Choka, alisema uwapo wa vifaa hivyo umerahisisha utendaji kazi katika hospitali hizo ambao kwa sasa nyaraka zote zinatunzwa kwenye kompyuta.

Alisema pia wameondokana na tatizo la foleni kwa wagonjwa ambao awali walikuwa wakikaa kusubiri majibu ya magonjwa yao.

Alisema kwa sasa hakuna foleni badala yake mgonjwa anachukuliwa vipimo na majibu yake huyapata kwa haraka zaidi kwa kuwa yanachakatwa kwa njia ya mtandao.

Baadhi ya wagonjwa waliopatiwa huduma katika Hospitali ya Rufani Mbeya, Juliana Philipo, alisema wanafurahia huduma zinazotolewa kwa sasa ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo awali.



Meneja programu anayeshughulikia masuala ya afya kutoka Shirika la GIZ, Kai Straehler (kulia), akimkabidhi vifaa vya TEHAMA Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Abeli Asilia (kushoto), kwa lengo la kurahisisha shughuli za utunzaji kumbukumbu na mtandao kiambo kwa hospitali na vituo vya afya vya mikoa ya Mbeya na Tanga vyenye thamani ya Sh. bilioni moja juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## RC Homera atambulisha mfumo ukusanyaji mapato kielektroniki

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametambulisha rasmi mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki wa maegesho ya vyombo vya moto kwenye hifadhi za barabara (TeRMIS), unaosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na kueleza faida lukuki zitokanazo na mfumo huo ikiwamo kuongeza ukusanyaji wa mapato nchini.

Homera alisema mfumo huo, unatarajiwa kuanza kufanya kazi rasmi Aprili mosi, mwaka huu na hakutakuwa na ukusanyaji wa fedha mkononi. Akizungumza mwishoni mwa wiki, Homera alisema mfumo huo wa ushuru wa maegesho kidijitali utasaidia kuziba mianya ya rushwa na kukuza uchumi wa nchi.

"Nawapongeza TARURA kwa ubunifu huu wa ukusanyaji wa vyanzo vya mapato kwa kufanya malipo ya ushuru wa maegesho ya vyombo vya moto ambao mtu atapaswa kulipa ushuru kupitia simu ya mkononi na baada ya malipo mteja atapokea ujumbe mfupi wenye uthibitisho wa malipo yake," alisema Homera.

Meneja wa TARURA, Mkoa wa Mbeya, Mwita Wilson, alisema miongoni mwa wadau waliopatiwa elimu kuhusu mfumo huo ni Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo ambao wameombwa kuwa mabalozi ili elimu hiyo iwafikie watu wengine.

Wilson alisema mfumo huo ni maalum kwa watumiaji wa vyombo vya moto kwenye maegesho ya hifadhi za barabara zilizojengwa na TARURA pamoja na TANROADS.

Aliwaomba watumiaji wa vyombo hivyo kutoa ushirikiano utakapoanza mfumo huo, Aprili mosi, mwaka huu ili kujenga uchumi wa nchi na kuwaletea wananchi maendeleo.

Akizungumzia mfumo huo, Ofisa Mawasiliano kutoka TARURA, Anitha David alisema, timu ya wataalamu iko mkoani Mbeya kwa ajili ya kutembelea maeneo yote pamoja na kutumia vyombo vya habari kutoa elimu ya namna mfumo huo utakavyofanya kazi.

Alisema mtumiaji wa maegesho ya vyombo vya moto atatakiwa kulipa ushuru wa maegesho ndani ya siku 14 tangu alipotumia maegesho na anatakiwa kulipa ushuru pamoja na faini ya Sh. 10,000.

# Taasisi zaombwa kudhibiti maambukizi kifua kikuu

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

IDADI kubwa ya wagonjwa wa kifua kikuu wilayani hapo, imeilazimu serikali kuziomba taasisi, watu binafsi na wadau wengine wa afya, kushirikiana kuukabili ugonjwa huo ili kupunguza kasi ya maambukizi ya kifua kikuu wilayani humo.

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma, Mkoa wa Mbeya, Dk. Osmunda Mwanyika, alisema hayo wakati wa mkutano wa kuhamasisha wananchi kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo, uliofanyika katika Kata ya Chimala.

"Katika mkoa wetu, wilaya ya Mbarali ndio inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa kifua kikuu mwaka 2021 watu 1,621 waligundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo kati ya 3,327 waliopimwa na kufikia asilimia 79," alisema Dk. Mwanyika.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mwanyika alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kujikinga na ugonjwa huo na kuhimiza matumizi sahihi ya dawa ili wapone.

Mwakilishi wa Shirika la MDH linaloratibu mradi wa kupambana na kifua kikuu mkoani Mbeya, Nickson Sam, alieleza jitihada zinazofanyika za kukabiliana na ugonjwa huo ambazo ni kufadhili mafunzo ya watoa huduma ya afya ya msingi 27 kwa halmashauri zote ili kwenda kuisaidia jamii dhidi ya mapambano ya kifua kikuu.

Alisema wahudumu wa afya ngazi ya jamii wameendelea kutembea kijiji kwa kijiji, nyumba kwa nyumba kutoa elimu kwa wananchi ili kujikinga na maambukizi ya kifua kikuu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliwaomba wagonjwa wa kifua kikuu kuendelea kutumia dozi za ugonjwa huo ili kupona kabisa badala ya kukatisha na kulimbikiza maambukizi ya ugonjwa.



## Miradi mikubwa kimkakati sasa yanukia Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imejipanga kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati katika kisiwa cha Pemba.

Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa Barabara Chakechake hadi Wete yenye urefu wa kilomita 22.1 ambayo itaiunganisha mikoa miwili ya Pemba.

Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alibainisha mpango huo alipotembelea miradi ya kimkakati ya serikali Pemba ikiwamo ujenzi wa Bandari ya Wete, mkoani na Shumba mjini.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ni muhimu katika kutimiza lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuifunguwa Pemba kuwa lango kuu la kiuchumi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Khatib, alisema ujenzi wa barabara hiyo ni muhimu ambayo unakwenda kuifunguwa Pemba kiuchumi katika maeneo huru ya kiuchumi.

"Ujenzi wa barabara hii umepokelewa kwa moyo mkunjufu na wananchi wa mkoa wa kaskazini Pemba kwa sababu unakuja kufungua Pemba katika uwekezaji kwa kutumia maeneo huru ya uchumi Micheweni," alisema.

Wakala wa barabara, Hassan Khamis, alisema ujenzi huo ulisimama kutokana na makubaliano ya mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) kuwa na masharti magumu katika utekelezaji wake.

**"Ujenzi wa barabara hii umepokelewa kwa moyo mkunjufu na wananchi wa mkoa wa kaskazini Pemba kwa sababu unakuja kufungua Pemba katika uwekezaji kwa kutumia maeneo huru ya uchumi Micheweni," alisema.**

# Makamu wa Rais asisitiza wanahabari wawezeshwe

**Na Rahma Sulleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema kuwa ili wanahabari kufanya kazi zao kwa ufanisi, hakuna budi kuwajengea mazingira wezeshi yatakayofanikisha utoaji wa habari bila pingamizi ama woga.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya wanasheria katika ukumbi wa Chuo cha Utalii Maruhubi Mjini Zanzibar yaliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Alisema pamoja na juhudi ziliopo, mazingira yanabainisha kuwa ni dhahiri bado sheria zina changamoto katika ufanisi wa habari na hivyo kusababisha uhuru wa habari kuwa mashakani.

Alieleza kuwa wakati umefika kufanya mapitio ya kina ya sheria inayohusiana na "Uchochezi" (sedition) ambapo nchi kadhaa zimefanya mapitio makubwa kuhusu mipaka, viini na vitendo mahsusi vinavyopelekea kosa la uchochezi.

Aidha alisema licha ya sheria hiyo kuainisha mipaka lakini bado inatoa fursa pana ya kutumika vibaya na vyombo vinavyosimamia sheria hasa Jeshi la Polisi.

"Hii ni moja ya sheria ambayo kwa jinsi ya ilivyo na mianya mingi ya kutumika vibaya inaweza kukwaza sio tu uhuru wa habari bali pia uhuru kwa ujumla wake. Tume za kupitia sheria za nchi kadhaa zimefanya tafiti nzuri juu ya sheria hii ambazo zinaweza kusaidia na hapa kwetu," alisema.

Othman aliishauri MCT kama waanzilishi wa mjadala pia kuja na mapendekezo yatayosaidia kuiweka nchi katika ramani ya kisasa ya uhuru wa habari.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa uhuru wa habari na kujieleza, Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, zimezungumzia kwa kina suala hilo, kama ambavyo inaonyesha Ibara ya 18 ya katiba hizo.

Alisema kwa kutambua uhuru huo, tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya awamu ya Nane, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekuwa akifanya mikutano ya wahariri na waandishi wa habari, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki yao ya msingi ya taarifa.

Alisema pia Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akiwaelekeza watendaji wake kushikirikiana na wanahabari katika majukumu yao, ambapo hivi karibuni vyombo vinne vya habari vilirejeshewa leseni za uendeshaji, baada ya kukaa kifungoni kwa vipindi tofauti.

"Nchi yetu imeingia mikataba kadhaa ya kimataifa na kikanda, inayosimamia na kubainisha haki ya raia ya kujieleza na kupata taarifa. Miongoni mwa hiyo ni mkataba maarufu wa haki za binadamu ambao umeelezea kwa kina haja ya kila nchi kuwa na uhuru wa habari," alisema.

Naye Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema, kuwa MCT inatekeleza mradi wa kukuza uhuru na usalama wa habari chini ya ufadhili wa nchini Swizalend ambao lengo lake ni kuweka mazingira mazuri kwa wanahabari kutekeleza majukumu yao.

Alisema katika mradi huo wanafanya kazi kwa pamoja kati ya Zanzibar na Bara kwa sababu masuala ya habari yanahusu pande zote mbili za Tanzania.

Meneja Rasilimali Watu wa MCT, Ziada Kilobo, alisema MCT itaendelea kutekeleza makujumu yao ikiwamo kusimamia maadili na weledi wa uandishi wa habari ili kuboresha sera na sheria za habari.




Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Mama Zainab Kombo Shaibu (kulia), akimkabidhi picha maalum mwenyekiti wa taasisi ya kusaidia yatima waishio majumbani Tanzania Taqwa Orphans Trust ambayo aliinunua mwenyekiti huyo kwa thamani ya shilingi laki tano, ikiwa ni mchango wake katika kusaidia futari kwa ajili ya yatima waishio majumbani wakati wa kongamano la kuchangisha futari, lililoandaliwa na taasisi hiyo katika ukumbi wa Golden Tulip Uwanja wa Ndege. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ataka bidii ya kazi kufikia malengo ya afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, ameitaka jumuiya ya kukuza na kuendeleza afya ya kinywa na meno Zanzibar inayojulikana kama Oral Health Development Organization (ZOHEDO) kufanyakazi kwa bidii ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar, wakati akizindua jumuiya hiyo na kuhakikisha inaenda sambamba na kauli mbiu 'isemayo jivunie uzuri wa kinywa chako kwa kuwa ndio haiba na ustawi wa afya yako'.

Alisema iwapo jumuiya hiyo itafanya kazi kwa pamoja na kujituma itafikia malengo waliokusudia na itaweza kuisaidia jamii kuibua matatizo yanayowakabili kiafya hasa katika tiba ya kinywa na meno.

Aidha, Naibu Waziri alisema kuwa katika sekta ya afya kuna baadhi ya watendaji hawawajibiki ipasavyo kwa kisingizio cha maslahi madogo jambo ambalo linarejesha nyuma malengo ya serikali ya kuinua sekta hiyo.

Naye Mkuu wa Afya ya Tiba ya Kinywa na Meno, Dk. Semeni Shaaban, aliomba serikali kuwapatia ajira vijana waliomaliza stashahada zao pamoja na eneo lenye vitendea kazi vya kisasa ili kufanya kazi kwa ufanisi kwa sababu jengo wanalotumia kwa sasa ni la kuazimwa.

Aidha, alifahamisha kuwa ili jumuiya hiyo iweze kuwa na ushirikiano mzuri na wizara na jumuiya zingine ni lazima kuwapo na mwakilishi ambaye atakayefanya kazi nzuri na kuleta maendeleo ya afya nchini.

Alisema afya ya kinywa na meno ni muhimu hivyo inapaswa kupewa kipaumbele kama maradhi mengine.

Akisoma risala kwa niaba ya jumuiya hiyo, Dk. Fatma Issa, alisema kuwa jumuiya inakabiliwa na ukosefu wa ofisi ya kufanyia kazi, wafadhili na daktari wa kinywa na meno.

Aidha alifahamisha kuwa jumuiya hiyo ni umoja ulioanzishwa kati ya wanafunzi na madaktari wote wa tiba ya kinywa na meno na kufanya tafiti nyingi nje na ndani ya Zanzibar ili kupeana habari.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

14/03/2022

ROBERTSON MICHAEL SIMBAGUE
S.L.P
KISARAWE.

YAH: KUKAMATA MALI YAKO VIWANJA VIWILIVIWILI NO.58 NA 59 VILIVYOPO KISARAWE MKOA WA PWANI DHIDI YA SHAURI LA MADAI NA. 96/2021 LINALOMHUSU
EDWARD E. LASWAI............................................MDAI
DHIDI YA
ROBERTSON M. SIMBAGIJE...........................MDAIWA

**Rejea kichwa cha habari hapo juu**

Nimeamriwa na mahakama ya Wilaya ya Kisarawe kupitia Mahakama Ya Mwanzo Kariakoo kukamata mali zako tajwa hapo juu dhidi ya shauri la Madai tajwa hapo juu.
Aidha Dalali Wa Mahakama nakupa siku 14 kuanzia taarifa ya barua hii uwe umelipa deni hilo kinyume cha hapo mali yako iliyokamatwa itauzwa kwa mnada kufidia deni hilo.

**Ndimi,**
PIUS T. MKUNDI
DALALI WA MAHAKAMA (M) PWANI

**Nakala:-**
-Mahakama Ya (W) Kisarawe
-Mahakama Ya Mwanzo Kariakoo
-Mwenyekiti Wa Serikali Ya Mtaa
-Edward E. Laswai

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

MODEY ENTERPRISES CO LIMITED anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye NAMBA ZA USAJILIMC 748CZU. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
TAARIFA YA POLISI: KAH /TR /RB/ 179/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

RIZWANA SHABBIR MUKADAMU anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya yenye NAMBA ZA USAJILI T 137 DJV. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
TAARIFA YA POLISI : KAH /TR /RB/ 161/2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 28-03-2022

### TANGAZO

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya ALHAMISI tarehe 31/03/2022. kampuni ya GIGA OIL COMPANY LIMITED itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka HORIRI BORDER kuelekea MOSHI kupitia HIMO .

1. Gari hizo zenye namba za usajili na vipimo vyake:

| | | | |
|---|---|---|---|
| I. T 648 ALN/ T485 BPF | UREFU 26 | UPANA 4.7 | KIMO 5.2 |
| II. T 718 BTC/ T874 CDS | UREFU 26 | UPANA 4.7 | KIMO 5.2 |
| III. T 600 BHU/ T476 CBG | UREFU 26 | UPANA 4.7 | KIMO 5.2 |

2. Gari hizo zinatoka HORIRI BORDER kuelekea MOSHI kupitia HIMO. Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka sasa 12:00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa Wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na..09..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ASHA H.MWALIKO WA K/NDEGE-MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HASSANI ABDALLAH MLANZI**

### TANGAZO
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 01 Mwezi 04 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 17 Mwezi 03 Mwaka 2022.

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA.**
**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA.**
**Usimamizi wa mirathi Na 41 /2022.**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU VERONICA R. GINGI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MATHIAS R. GINGI**

### TANGAZO
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 mwezi 04 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 03 mwaka 2022.

..................................................................
**HAKIMU**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HOME AFFAIRS**
**IMMIGRATION DEPATMENNT**

Telegram: IMMIRATION
Simu 027-2503569
In reply please quote:
REG: AR/REG/08/VO.X. I 18989

Ofisi ya Uhamiaji Mkoa,
S.L.P.236,
ARUSHA
24.03.2022

### APPLICATION FOR CITIZENSHIP



Notice is hereby given that,
Mr/Mrs/Miss MARY PRISCILLAH WAHU MURITU

Whose photograph is provide above,is applying to the Minister for Home,Affairs for Tanzania Citizenship.His/Her Nationality at present is KENYA The country of origin is KENYA Her occupation is TEACHER Hisemployer/ Business/Address is She has been in this country since 2006 apart from ARUSHA Region,she has also resided in ARUSHA Region.

That,any person who knows any reason why citizenship should not be granted to the applicant, should sent a written and signed statement of facts to the commissional General of Immigration Services,P.O.BOX 512,DAR –ES-SALAAM. Using Ref. No. AR/DN/18989

**FOR : COMMISSIONER GENERAL OF IMMIGRATION SERVICES**

**JAMHURI YA MAHAKAMA WA TANZANIA**
**(MAHAKAMA)**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO INABOISHU WILAYA YA ARUMERU**

**SHAURI LA JINAI /MADAI NA 112 YA 2021**

**ARUSHA VICTORY PRE AND PRIMARY SCHOOL.............. MDAI/MLALAMIKIWA**

**DHIDI YA**

**ELINEEMA KALALU............ MDAIWA/MSHITAKIWA**

**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMONS GENERAL)**
**(MCA Na 2/1984)**

**Kwa ELINEEMA KALALU**
**KONGOWE (DSM)**

Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ujibu shtaka/madai kuwa shahidi kama ifuatavyo **FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA,UNAAMRIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya Ijumaa tarehe 8/4/2022 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa .

**USIKOSE KUHUDHURIA**
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kutokuhudhuria mahakamani ni kosa k/ 1 Na 114 A sura 16 K/A. Hivyo mahakama yaweza kuchukua hatua za kisheria.
**HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO 07/03/2022.**

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LODRICK IMMANUEL URONU**
Anatangaza kupotolewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.363 AUN** aina ya **NISSAN CEFIRO.**
Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi.
**KAH/ TR/RB/1863 /2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 463 YA Mwaka 2021**

**BAINA YA**
**MAGRETH MSUTA ........................................MDAI**

**DHIDI YA**

**MASHAKA SABINI KIHAMA........................MDAIWA**

### YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 11.05.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANAGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 25 ya mwezi March,2022.

COURT SEAL DODOMA DISTRICT
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT
..................................
RESIDENT MAGISTRATE


# NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI KIMATAIFA

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE

## Ukraine yafikiria kuitisha kura ya maoni iwapo ijiunge na NATO

**Kyiv, UKRAINE**

IKIWA ni takribani siku 34 tangu Russia ilipoanza kuishambulla Ukraine, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, amesema vipaumbele katika mazungumzo kati ya Ukraine na Russia, vitazingatia uhuru na mamlaka ya mipaka ya nchi yake.

Ameyasema hayo katika ujumbe wa video na kuongeza kuwa ipo fursa na haja ya mkutano wa ana kwa ana na Russia nchini Uturuki, ambako duru nyingine ya mazungumzo kati ya pande hizo mbili inatarajiwa kufanyika wiki hii.

Zelenskiy pia amewaambia waandishi wa Russia, kwamba serikali yake itazingatia kutangaza kutoegemea upande wowote na kutoa hakikisho la usalama kwa Russia, ambao utahusisha Ukraine kutokuwa na silaha za nyuklia.

Alisema suala la kutoegemea upande na kuachana na mipango ya kujiunga na Jumuiya ya Kujihami (NATO), yanapaswa kuamuliwa na raia kupitia kura ya maoni.

Alisisitiza itafanyika hivyo baada ya vikosi vya Russia, kuondoka nchini mwake.

Mazungumzo kati ya nchi hizo mbili yanataraji kuanza jijini Istanbul nchini Ukraine.

Timu za upatanishi kutoka upande wa nchi hizo, jana, zilitarajiwa kuanza mazungumzo ya amani kwa siku mbili, kwa mujibu ofisa mwandamizi wa Uturuki.

Hata hivyo taarifa hiyo haikuwa na ufafanuzi zaidi, ingawa katika mazungumzo yao kwa njia ya simu mwishoni wa wiki, Rais Recep Tayyip Erdogan wa Uturuki na mwenziwe wa Russia, Vladimir Putin walikubaliana kufanyika kwa mazungumzo hayo ambayo serikali ya Ankara ina matumani kuwa yanaweza kufanikisha hatua ya kuwekwa chini silaha.

Awali kabla ya taarifa hiyo, mmoja wa maofisa waandamizi wa Ukraine, mshauri katika Wizara ya Mambo ya Ndani, akiwa pia mwakilishi wa Ukraine katika mazungumzo hayo, Vadym Denysenko alitoa kauli ya kukatisha tamaa akisema hatarajii matokeo makubwa ya kupatikana katika mazungumzo hayo.

Kimsingi Uturuki vilevile imezuia shughuli za uvuvi katika nyakati za usiku katika eneo lake la bahari la Kaskazini/Magharibi, hadi itakapoamua vinginevyo.

Russia na Ukraine, zimekuwa zikitupiana lawama za kutega mabomu katika eneo la Bahari Nyeusi.

Watu 160,000 bado wamekwama katika mji uliozingirwa wa Mariupol, huku kukiwa bado kuna shida kadhaa ikiwamo ya umeme.

Ofisi yenye kushughulika na haki za binadamu katika Umoja wa Mataifa inasema watu 1,119 wameuawa na wengine 1,790 wamejeruhiwa tangu kuzuka kwa mapigano nchini Ukraine.



Rais wa Marekani, Joe Biden, akiwa na Waziri Mkuu wa Poland, Mateusz Morawiecki (kushoto), akimbeba mtoto kutoka Ukraine katika Uwanja wa Taifa PGE, mjini Warsaw, nchini Poland, jana. **PICHA: REUTERS**

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

## Idadi wanasiasa kuhama vyama yaongezeka

**Nairobi, KENYA**

WAKATI Kenya ikitarajia kufanya uchaguzi mkuu Agosti mwaka huu, vuguvugu linapamba moto kisiasa huku takriban nusu ya wabunge Kenya, wakitarajiwa kuhama kwenye vyama vyao na kujiunga na vyama vingine vya siasa wakati wakiomba kuchaguliwa tena katika uchaguzi ujao wa Agosti.

Kabla ya tarehe ya mwisho ya Machi 26, mwaka huu, kwa vyama kuwasilisha orodha ya wanachama wao kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, kiasi cha wanachama 180 wa Bunge la Taifa na Baraza la Seneti, wametangaza hadharani kuhama katika vyama vilivyowadhamini katika uchaguzi wa 2017, idadi hiyo ikitegemewa kuongezeka.

Tayari kuna wanachama 416 katika mabunge mawili ya taifa, ikiwamo wale walioteuliwa kuwakilisha makundi maalum kama vile vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Kuhama kwa idadi kubwa ya wanachama hakujaiacha serikali za ugatuzi, huku sio chini ya magavana wa Kaunti 15 kati ya 26 wa awamu ya kwanza, ambao wanatakiwa kuchaguliwa tena mwaka huu, wamebadilisha ushirika wao na chama.

Kwa mujibu wa sheria mpya iliyopitishwa Februari, wagombea kwa nafasi mbalimbali za kuchaguliwa lazima wathibitishe uanachama wao wa chama ifikapo Machi 26, mwaka huu, ili kuweza kukidhi uhalali wa kugombea katika uchaguzi wa awali wa chama mwezi Aprili.

Sheria hiyo inawaruhusu wale ambao hawana mafungamano na chama cha siasa kugombea kwa nafasi binafsi.

Wengi kati ya wanasiasa wanaohama kwenda vyama vipya wanaona tiketi mbadala ya kugombea inawapa fursa nzuri zaidi ya kushinda.

Kadhalika, baadhi hawana imani kuwa vyama vyao vitaendesha uchaguzi wa awali wa haki.

Kuhama kwao katika msimu huu, kunaonyesha nchi inavyohangaika na demokrasia ya vyama vingi.

Hakuna rais aliyegombea au kutetea nafasi yake kwa kutumia chama kile kile au muungano ule ule, kwa chaguzi nne zilizopita.

Wakenya watapiga kura katika uchaguzi wa saba katika kipindi cha miaka 30, tangu kuanzishwa tena kwa mfumo wa siasa za vyama vingi.

Nchi hiyo ilikuwa imetangazwa kuwa ni taifa la chama kimoja mwaka 1982, miaka iliyofuatia, vyama vya siasa ambavyo vimejitokeza kwa ajili ya kipindi cha uchaguzi vimeonekana kuwa dhaifu kwa kukosekana shinikizo la maadili, kama vile soko huru na itikadi mbalimbali za kisoshalisti.

Vyama vinne vikuu katika uchaguzi mkuu wa 1992, Kanu, Ford Kenya, Ford Asili na chama cha Demokratik, ni kivuli cha vyama vilivyokuwapo awali.

Kanu, chama cha tangu uhuru na kilichoshinda viti 100 vya bunge mwaka 1992 chini ya uongozi wa Rais Daniel Arap Moi, hivi sasa kina viti 10 tu katika Bunge la Taifa lililoongezeka.

Ford-Kenya ni chama pekee kingine katika kizazi kilichotangulia, nacho kimeshuhudia kupungua kwa idadi ya viti vyake bungeni kutoka 31 mwaka 1992 hadi 12 hivi sasa.

Hivi karibuni, vyama vya siasa vimejikuta vikihangaika kujitambulisha, kwa sababu ya kuongezeka muungano wa vyama, kwa kiwango kikubwa ushirikiano wa kikabila kwa haraka wakijikusanya kama chombo chenye lengo la kushinda uchaguzi.

Wengi wao kati ya wale wanaohama vyama hivi sasa wanabadilisha mahusiano yao, kwenda chama cha muungano wa Azimio la Umoja, linalohusishwa na Rais Uhuru Kenyatta na mrithi wake anayetakiwa, Raila Odinga, au chama cha Kenya Kwanza Alliance. kinachoongozwa na Makamu wa Rais, William Ruto.

Muungano wa pande hizo mbili, umefanyika katika kipindi cha miezi miwili iliyopita.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RAPHINA SAFI BARCA

BARCELONA wamefikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, kuhusu uhamisho wa kutoka Leeds United msimu huu wa majira ya joto. ***(Sport)***

### BARCA KUACHIA WACHEZAJI

BARCELONA wako tayari kuwaachia wachezaji saba msimu huu wa majira ya joto kuondoka katika klabu hiyo wanapojiandaa kuimarisha kikosi chao, huku mlinzi wa Chelsea, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32, na beki Andreas Christensen mwenye miaka 25 wakihusishwa na uhamisho hapo Nou Camp. ***(AS)***

### DEPAY KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 kutoka Barcelona. ***(Mundo Deportivo)***

### RICE NAHODHA ENGLAND

KIUNGO wa kati wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23, anapigiwa upatu kuwa nahodha wa timu ya Taifa ya England, kwa mujibu wa kocha, Gareth Southgate. ***(Mirror)***

### TIERNEY ATAKIWA MADRID

REAL Madrid wanaandaa dau la pauni milioni 50 kumnunua mlinzi wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 24**.** ***(Sunday Post)***

### MAITLAND-NILES AWINDWA

KLABU za Ligi Kuu England, zinatazamiwa kuwa macho na mchezaji wa kimataifa wa England, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 24, ambaye hatarajiwi kubakishwa na Klabu ya AS Roma kwa mkopo baada ya msimu huu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### TCHOUAMENI ANUKIA CHELSEA

CHELSEA wameimarika katika harakati zao za kumnasa Aurelien Tchouameni baada ya wakala wa kiungo huyo wa kati wa Monaco na Ufaransa kukanusha kuwa wana makubaliano na Real Madrid. ***(Le Parisien, via Fabrizio Romano)***

### OSIMHEN AWEKEWA BEI

KLABU ya Napoli imeweka bei ya pauni milioni 83 kwa mshambuliaji wao raia wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23. ***(Corriere dello Sport, via Sun)***

### SCHJELDERUP KAIKATAA LIVER

NYOTA wa Norway anayechipukia, Andreas Schjelderup mwenye umri wa miaka 17, amesema alikataa fursa ya kusajiliwa na Liverpool, lakini kiungo huyo ameacha milango wazi kwa uwezekano wa kuhama katika siku zijazo. ***(Liverpool Echo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA: BADO SIJAFANYA MAAMUZI YOYOTE UNITED

●●●Naweza kuamua kesho au siku ya dirisha la usajili, nataka kumaliza msimu vizuri, lakini...

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Klabu ya Manchester United, Paul Pogba, amesema bado hajafanya maamuzi yoyote ikiwa atabaki au ataondoka huku mkataba wake ukitarajiwa kuisha Juni na kuwa mchezaji huru.

Pogba, ambaye kwa sasa ana miaka 29, amekuwa mchezaji kijana zaidi kufikisha michezo 90 ambayo ameichezea timu ya Taifa ya Ufaransa, Ijumaa iliyopita.

"Sijafanya maamuzi yoyote hadi sasa, hakuna kilichofanyika. Naweza kuamua kesho, naweza kuamua siku ya dirisha la usajili tu, nataka kumaliza msimu vizuri.

"Huu msimu bado haujaisha, lakini hatupo kwenye nafasi yoyote ya kuweza kushinda taji lolote, nahitaji kushinda mataji, kucheza kwa ajili ya kitu fulani, lakini kwa mwaka huu na miaka michache iliyopita hatujafanikiwa kushinda taji lolote, inakatisha moyo.

"Kucheza kwenye timu ya taifa kunanipa amani, huo ndio ukweli. Kulikuwa na kipindi kigumu kwa kipindi fulani pale United na nilihitaji haya mapumziko ili kuweza kupata hii nguvu na hali ya kujiamini.

"Kuna muda nilikuwa sichezi au matokeo mabovu, kuja hapa, inaniamsha morali, kuweza kupumzika na kupumua kunanisaidia mimi kurudi vizuri kwenye klabu."

Pogba ni miongoni mwa wachezaji watano ambao mikataba yao inamalizika pale Man United akiwamo, Jesse Lingard, Juan Mata na Edinson Cavani.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 1,089

MECHI KALI
SENEGAL
VERSUS
EGYPT
1 | 1.89
X | 2.87
2 | 4.48

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ERIKSEN: NAJIHISI KAMA MCHEZAJI TENA



**COPENHAGEN, Denmark**

NYOTA wa Klabu ya Brentford na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen, ameshindwa kuficha furaha yake baada ya kufunga bao kwenye mchezo wake wa kwanza wa kimataifa tangu apatwe na shambulio la moyo, licha ya Denmark kufungwa 4-2 na Uholanzi.

Eriksen amekuwa nje ya uwanja kwenye michezo ya kimataifa kwa siku 287, baada ya kupata matatizo ya moyo katika mchezo wa ufunguzi kwenye kundi lao katika michuano ya Euro 2020.

Eriksen amefanikiwa kufunga kwenye mchezo huo ndani ya dakika mbili baada ya kuingia na kushindwa kuizuia furaha yake pale alipohojiwa na alinukuliwa akisema, "najihisi kama mchezaji tena, nimekuwa nje ya uwanja kwenye michezo ya kimataifa kwa muda mrefu sana.

"Nina furaha kurudi tena, kufanikiwa kufunga kumeniongezea furaha zaidi, inanipa hisia nzuri.

Ni vizuri nimefanikiwa kufunga, lakini ningeweza kufunga bao lingine la pili. Nilikuwa na miaka bora hapa na nakumbuka goli lilipo kwenye uwanja huu."

# Hazard kupasuliwa tena

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Real Madrid, Eden Hazard anatarajia kufanyiwa upasuaji mwingine kwenye mguu wa kulia, hivyo kutarajiwa kuwa nje ya dimba kwa mwezi moja.

Hazard ambaye alisajiliwa kwa ada ya uhamisho wa pauni milioni 98 akitokea Chelsea mwaka 2019, amefanikiwa kucheza michezo 65 tu, huku akishindwa kupata namba ya kudumu kwenye kikosi cha 'Los Blancos' hao kutokana na kupata majeraha ya mara kwa mara.

Majeraha ya sasa yatamweka nje ya kikosi cha Real Madrid ambacho kitacheza dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi ujao.

Hazard atafanyiwa upasuaji kwenye mguu wake wa kulia baada ya kuvunjika Machi 2020.

"Kwa siku kadhaa zijazo, mchezaji wetu Eden Hazard, atafanyiwa upasuaji wa mguu wa kulia," taarifa ya klabu hiyo ilisema.

Hazard amecheza michezo 22 tu msimu huu huku akianza kwenye mechi nane za LaLiga wakati akifunga bao moja na kusaidia kupatikana mawili, pia hajafanikiwa kucheza tena tangu alipoingia kwenye mchezo dhidi ya Alaves Februari 19, mwaka huu.



## HABARI MICHEZO


9,062,840

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/04/22 | 17:00 | Leeds vs Southampton | 2.36 | 3.53 | 2.83 |
| 02. 02/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 2.84 | 3.09 | 2.54 |
| 03. 02/04/22 | 19:30 | Borussia Dortmund vs RB Leipzig | 2.38 | 3.59 | 2.69 |
| 04. 03/04/22 | 14:00 | Rangers vs Celtic | 2.36 | 3.28 | 2.88 |
| 05. 03/04/22 | 15:30 | Fortuna Sittard vs Heracles Almelo | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 06. 03/04/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.56 | 2.96 | 2.96 |
| 07. 03/04/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Nantes | 2.55 | 3.05 | 2.90 |
| 08. 03/04/22 | 16:00 | Atalanta vs Napoli | 2.42 | 3.20 | 2.90 |
| 09. 03/04/22 | 16:30 | Augsburg vs VfL Wolfsburg | 2.86 | 3.26 | 2.45 |
| 10. 03/04/22 | 19:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.59 | 3.03 | 2.79 |
| 11. 03/04/22 | 19:30 | Granada vs Rayo Vallecano | 2.68 | 3.13 | 2.73 |
| 12. 03/04/22 | 20:00 | Moreirense vs Vitoria Guimaraes | 2.80 | 3.20 | 2.47 |
| 13. 03/04/22 | 21:45 | Juventus vs Inter | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.


JUMANNE - 29/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:35 | 5417 | Japan vs Vietnam | 1.11 | 7.01 | 17.54 |
| 14:30 | 4068 | Iran vs Lebanon | 1.25 | 4.87 | 10.72 |
| 15:00 | 4558 | QPR U23 vs Charlton U23 | 2.26 | 3.70 | 2.58 |
| 15:30 | 1325 | Persepam MU vs PS Tni | 3.05 | 2.72 | 2.47 |
| 16:45 | 1603 | United Arab Emirates vs South Korea | 3.97 | 3.39 | 1.81 |
| 16:45 | 2712 | Syrian Arab Republic vs Iraq | 3.51 | 2.87 | 2.14 |
| 17:00 | 2234 | Poland U21 vs Hungary U21 | 1.40 | 4.49 | 6.05 |
| 17:00 | 2485 | Kazakhstan vs Moldova | 2.20 | 2.95 | 3.60 |
| 17:00 | 3390 | Slovakia U21 vs Spain U21 | 4.47 | 4.08 | 1.58 |
| 17:00 | 3516 | Croatia vs Bulgaria | 1.43 | 4.24 | 7.88 |
| 17:00 | 3650 | Serbia U21 vs Armenia U21 | 1.14 | 6.80 | 13.61 |
| 17:00 | 5787 | Wales U21 vs Bulgaria U21 | 2.12 | 3.36 | 3.02 |
| 18:00 | 2350 | Israel U21 vs Germany U21 | 5.62 | 4.46 | 1.43 |
| 18:30 | 2150 | Italy U21 vs Bosnia and Herzegovina U21 | 1.18 | 5.84 | 12.65 |
| 19:00 | 1106 | Finland vs Slovakia | 2.87 | 3.17 | 2.52 |
| 19:00 | 1914 | Oman vs China | 1.81 | 3.25 | 4.18 |
| 19:00 | 2222 | Greece U21 vs Portugal U21 | 5.26 | 3.90 | 1.53 |
| 19:00 | 2227 | Denmark vs Serbia | 1.92 | 3.34 | 4.15 |
| 19:00 | 2262 | Cyprus vs Estonia | 2.69 | 2.84 | 2.89 |
| 19:00 | 2358 | Andorra U21 vs Czech Republic U21 | 15.51 | 8.14 | 1.10 |
| 19:00 | 3566 | Croatia U21 vs Finland U21 | 1.41 | 4.47 | 6.02 |
| 19:00 | 5519 | Switzerland vs Kosovo | 1.34 | 4.86 | 9.51 |
| 19:45 | 2822 | Netherlands U21 vs Switzerland U21 | 1.52 | 4.11 | 5.08 |
| 20:00 | 1553 | Senegal vs Egypt | 1.89 | 2.87 | 4.48 |
| 20:00 | 2199 | Nigeria vs Ghana | 2.04 | 2.82 | 3.89 |
| 20:00 | 2558 | Norway vs Armenia | 1.37 | 4.65 | 8.90 |
| 20:30 | 2294 | Qatar vs Slovenia | 2.44 | 3.18 | 2.98 |
| 20:45 | 3433 | Israel vs Romania | 2.57 | 3.03 | 2.93 |
| 21:00 | 1952 | Denmark U21 vs Belgium U21 | 2.68 | 3.26 | 2.38 |
| 21:00 | 2041 | Saudi Arabia vs Australia | 2.48 | 3.02 | 2.73 |
| 21:45 | 1190 | Poland vs Sweden | 2.45 | 3.02 | 3.12 |
| 21:45 | 2090 | Turkey vs Italy | 3.80 | 3.36 | 2.00 |
| 21:45 | 2400 | England vs Ivory Coast | 1.49 | 4.18 | 6.64 |
| 21:45 | 2479 | Albania U21 vs England U21 | 8.54 | 5.63 | 1.24 |
| 21:45 | 2514 | Northern Ireland vs Hungary | 2.53 | 3.09 | 2.93 |
| 21:45 | 2535 | Oldham vs Leyton Orient | 3.42 | 3.32 | 2.06 |
| 21:45 | 3172 | Spain vs Iceland | 1.22 | 6.06 | 13.12 |
| 21:45 | 3249 | Salford City vs Crawley Town | 1.87 | 3.36 | 4.05 |
| 21:45 | 3452 | Hartlepool vs Mansfield | 2.97 | 3.17 | 2.34 |
| 21:45 | 3576 | Belgium vs Burkina Faso | 1.10 | 9.06 | 26.17 |
| 21:45 | 3669 | Ireland vs Lithuania | 1.38 | 4.63 | 8.45 |
| 21:45 | 4195 | Wales vs Czech Republic | 2.47 | 3.24 | 2.89 |
| 21:45 | 4345 | Austria vs Scotland | 2.04 | 3.33 | 3.73 |
| 21:45 | 5060 | Rochdale vs Carlisle | 2.03 | 3.37 | 3.42 |
| 21:45 | 5498 | Portugal vs North Macedonia | 1.19 | 6.44 | 16.09 |
| 21:45 | 5853 | Netherlands vs Germany | 2.57 | 3.28 | 2.73 |
| 22:15 | 4682 | France vs South Africa | 1.19 | 6.27 | 16.17 |
| 22:30 | 2648 | Morocco vs DR Congo | 1.52 | 3.61 | 6.05 |
| 22:30 | 5075 | Tunisia vs Mali | 2.38 | 2.72 | 3.20 |
| 22:30 | 5621 | Algeria vs Cameroon | 2.04 | 2.82 | 3.89 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MWAKINYO AJIFUA NA MKALI WA MASUMBWI MAREKANI

**Na Cheji Bakari, Tanga**




BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, yupo Jimbo la California, Marekani kwa takriban mwezi mzima sasa akifanya mazoezi binafsi chini ya bondia maarufu wa zamani wa ngumi za kulipwa, Bernard Hopkins Jr.

Mwakinyo ambaye hivi karibuni alipanda viwango na kuwa katika nafasi ya 14 duniani na nafasi ya kwanza Afrika katika uzani wa super welterweight kwa mujibu wa mtandao wa www.boxrec.com, juzi alitupia baadhi ya video fupi na picha za mnato akifanya mazoezi kupitia akaunti yake ya Instagram ya mwakinyopros akiwa na bondia huyo ambaye alianza ngumi mwaka 1988.

Hopkins Jr maarufu 'Executioner' (Mnyongaji), alionekana akimpa mazoezi mbalimbali ya stamina, kurusha na kukinga makonde na ya pumzi.

Gazeti hili lilipomtafuta 'inbox' kutaka kujiridhisha kwamba ni kweli yupo nchini humo na anatarajia kurejea lini, hakutoa maelezo marefu zaidi ya kujibu tu kwa ufupi.

"Nipo Marekani takriban mwezi sasa pamoja na mambo mengine pia nakutana na wazoefu kufanya mazoezi na kunipa ujuzi."

Mwakinyo alipanda ulingoni mara ya mwisho Septemba 3, mwaka jana, dhidi ya bondia kutoka Namibia, Julius Indongo kugombea Mkanda wa ABU katika pambano la raundi 12 la uzito wa Superwelt Weight ambalo alimshinda kwa TKO.

Mwakinyo ana miaka mitano tangu alipoanza kucheza ngumi za kulipwa na amecheza jumla ya mapambano 22, ameshinda 20 na kupoteza mawili.

# Kagera yaipigia mahesabu Mtibwa

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Kagera Sugar kimeingia kambini kujiandaa na mechi ya 'Dabi ya Wakulima wa Miwa' dhidi ya Mtibwa Sugar inayotarajiwa kupigwa Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hamisi Mazanzala, amesema kikosi chao kimeingia kambini na kuanza mazoezi Jumapili iliyopita chini ya Mkenya Francis Baraza kujiandaa na mechi hiyo ambayo amesema itakuwa ngumu kwa sababu timu hizo zina undugu na zinafahamiana.

"Tumeshaanza maandalizi, tuna siku kama saba hivi ya kurekebisha makosa chini ya Baraza, tunajua kuwa



tuliwafunga Mtibwa Sugar kwenye mechi ya kwanza walipokuja hapa Kaitaba, lakini hii haitufanyi tuwadharau kwa sababu hivi sasa wamebadilika sana, hivyo mechi itakuwa ngumu, tena wao watakuwa nyumbani," alisema Mazanzala.

Kuhusu ligi kwa ujumla, Ofisa Habari huyo amesema kocha wao ameonekana bado hajafurahishwa na nafasi waliyopo kwani tofauti ya pointi si kubwa kwa timu za kati na za chini, hivyo amewahimiza wachezaji wake kupambana zaidi.

"Kawaambia wachezaji kuwa ligi ya msimu huu ni ngumu, ukishinda leo unapanda juu sana, ukifungwa unarudi chini sana kwa sababu pointi zinapishana kidogo tu kuanzia timu za kati mpaka chini kwa hiyo anataka timu izidi kwenda juu," alisema.

Kagera Sugar inashika nafasi ya sita ikiwa na pointi 24 kwa mechi 18 ilizocheza, huku Mtibwa ikiwa kwenye nafasi ya 14 kwa pointi zake 19.

# Michezo

Jumanne Machi 29, 2022
Nipashe



Poulsen aahidi mabadiliko Stars ikiivaa Sudan

NAMNA HII...



Mshambuliaji wa Simba, Denis Kibu akimiliki mpira dhidi ya beki wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala' wakati wa mazoezi. Kushoto ni Joash Onyango. Timu hiyo inajiandaa na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Gendarmerie ya Niger itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili. **PICHA: MAKTABA**

# CAF YAISHUSHIA RUNGU BERKANE MECHI SIMBA

## Yapigwa faini milioni 249, ni kwa kufanya vurugu Morocco hadi kwa Mkapa Dar, kiongozi wao afungiwa...

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Nidhamu ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), imeishushia rungu zito Klabu ya RS Berkane ya Morocco kutokana na kufanya vurugu kwenye mechi dhidi ya Simba ikiwa nyumbani nchini kwao na katika mechi ya marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Machi 13, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na CAF jana kupitia mtandao wao, imeitoza RS Berkane jumla ya dola za Kimarekani 108, 000 sawa na shilingi 249,738,120 za Tanzania huku ikimfungia kiongozi wao mmoja, Majid Madrane kwa mwaka mmoja kutojihusisha na mchezo wa soka kutokana na kuongoza vurugu katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Taarifa ya CAF kupitia mtandao wao wa online, imesema kuwa imemfungia ofisa huyo kwa kuvamia uwanja na kuwachochea wachezaji wa RS Berkane kuungana naye kwenda kumshambulia mwamuzi Jacques Ndala kwenye mechi hiyo iliyoisha kwa Simba kushinda bao 1-0, kiasi cha kusababisha mechi kusimama kwa dakika tano.

Kutokana na tukio hilo, taarifa hiyo ikafafanua kuwa klabu hiyo imetozwa faini ya dola za Kimarekani 100,000 ambazo ni sawa na shilingi 231,239,000 za Tanzania.

Lakini taarifa hiyo, imeongeza kuwa imeitoza pia RS Berkane kiasi cha dola la Kimarekani 8,000 sawa na shilingi 18,499,120 za Tanzania baada ya mashabiki wake kuruka uzio na kuingia uwanjani wakati wa mechi yao dhidi ya Simba iliyochezwa Februari 27, mwaka huu, nchini Morocco, wakishinda mabao 2-0, hivyo kutakiwa kulipa jumla ya dola 108,000 sawa na Sh. miliomi 249.7 za Tanzania.

Katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam, viongozi na wachezaji wa RS Berkane walionekana kutoridhishwa na maamuzi ya mwamuzi, Ndala kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kusababisha kashikashi za hapa na pale, huku mpira ukisimama mara kwa mara.

Na baada ya mchezo huo, uongozi wa RS Berkane uliweka wazi kuwa ulikata rufani CAF ukimlalamikia Ndala kuwa hakuchezesha kwa haki mchezo huo.

Lakini hilo halikuizuia CAF kuchunguza na kuchukua hatua hiyo, lakini ikaonyesha kwamba Ndala ni mmoja kati ya waamuzi bora inaowakubali kwa kumpanga kuchezesha mechi kali ya mchujo kati ya Misri na Senegal kuwania kufuzu Fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Simba na Berkane kila moja itakuwa nyumbani Jumapili wiki hii kuhitimisha mechi za hatua ya makundi kwa kuzikaribisha Gendarmerie na Asec Mimosas, zote zikihitaji kushinda ili kutinga robo fainali.

Asec inaongoza Kundi D ikiwa na alama tisa, hivyo itahitaji sare ama ushindi wakati wenyeji wao Berkane ushindi pekee ukiwa ndio tiketi yao ya kuweza kutinga robo fainali kama ilivyo kwa Simba ambayo itahitaji kushinda dhidi ya Gendarmerie ili kusonga mbele.

# Fei Toto nje wiki 6, Moloko arejea

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI winga wa Yanga raia wa DR Congo, Jesus Moloko, ambaye alikuwa majeruhi kwa majuma kadhaa, amepona na ameanza mazoezi na wenzake kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, kiungo fundi wa Wanajangwani hao, Feisal Salum 'Fei Toto', atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha wiki sita, imeelezwa.

Yanga itakuwa ugenini Aprili 6, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kuwavaa wenyeji Azam FC bila Fei Toto.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuelekea mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Sudan itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo, Kocha wa Taifa Stars, Kim Poulsen alisema katika mchezo huo atamkosa Fei Toto', ambaye amegundulika ni majeruhi na kutakiwa kukaa nje kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa daktari wa timu ya Taifa, Lisobine Kisongo, Fei Toto tayari ameruhusiwa kurejea klabuni kwenda kutibiwa na hatakuwapo katika kikosi cha Stars kwa sababu ya majeraha makubwa ya msuli wa ndani ambayo yatamweka nje ya dimba kwa kipindi cha wiki sita.

"Katika uchunguzi wetu tumegundua Fei Toto aliumia muda mrefu tangu Januari 26, mwaka huu akiwa na klabu yake ya Yanga, alipokuja Stars alifanyiwa uchunguzi na kubainika ana tatizo, hivyo anatakiwa kufanyiwa matibabu ya kina," alisema.

Kuhusu kurejea kwa Moloko, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema mbali nyota huyo raia wa DR Congo, mchezaji mwingine aliyekuwa majeruhi kwa muda mrefu, Yacoub Songne naye baada ya siku tatu, ataanza mazoezi na wenzake kwani naye ameshapona, ila kuna mambo mawili matatu ya kimatibabu ambayo anamalizia.

"Tunashukuru Mungu kwa sasa lile jinamizi la majeruhi tunalimaliza, Jesus Moloko amepona kabisa na ameanza mazoezi, kwa hiyo tunatangaza rasmi urejeo wake, Yacouba Songne naye atarejea mazoezini baada ya siku mbili tatu hivi, kwa hiyo tunaelekea kulimaliza lile jinamizi la majeruhi yaliyokuwa yakitukabili," alisema Bumbuli.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042